Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

# Ripoti ya Takwimu ya Sekta ya Mawasiliano

Robo ya mwaka inayoishia Desemba 2025

www.tcra.go.tz

VIWANGO VYA ISO 9001: 2015

Toleo 1.0

# Muhtasari

Ripoti hii inatoa takwimu za mawasiliano ya simu na intaneti, utangazaji, posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto. Takwimu zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vya Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU) vya kukusanya na kuandaa takwimu za huduma ya mawasiliano/TEHAMA.

Kwa kipindi cha robo mwaka iliyoishia Desemba 2025, huduma za mawasiliano ya simu zimeonesha ukuaji mkubwa zikiwa na ongezeko la usajili wa laini la asilimia 7.7 kutoka milioni 99.3 katika robo mwaka iliyoishia Septemba 2025 na kufikia milioni 106.9 . Mkoa wa Dar es Salaam umeendelea kuwa soko kubwa zaidi nchini ukiwa na laini za simu milioni 19.68. Vilevile, usajili wa intaneti umeongezeka kwa asilimia 3.2 kutoka laini milioni 56.3 katika robo mwaka iliyoishia Septemba 2025 na kufikia laini milioni 58.1, na matumizi ya huduma za intaneti yameongezeka kwa asilimia 9.5 kutoka petabytes 738 katika robo mwaka iliyoishia Septemba 2025 na kufikia PetaBytes 808. Intaneti ya kasi imeendelea kuwa njia inayopendelewa zaidi kupata intaneti ikichangia asilimia 56 ya usajili wote wa intaneti. Wakati idadi ya dakika ndani ya nchi ikipungua kwa asilimia 0.3, idadi ya jumbe fupi (SMS) iliongezeka kwa asilimia 9.2.

Kiwango cha upenyo wa simu janja kimeongezeka kufikia asilimia 41.82 na simu za rununu kufikia asilimia 87.11. Ukuaji huu umechangiwa na uendelezwaji wa miundombinu unaodhihirishwa na ongezeko la idadi ya minara kutoka 9,745 katika robo mwaka iliyoishia Septemba 2025 na kufikia minara 10,029, pamoja na ongozeko la asilimia ya watu waliofikiwa na mtandao wa 5G kutoka asilimia 28.9 katika robo mwaka iliyoishia Septemba na kufikia asilimia 30.1.

Katika sekta ya utangazaji, idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa imepungua kwa asilimia 8.5 kutoka visimbuzi milioni 2.3 katika robo mwaka iliyoishia Septemba 2025 na kufikia visimbuzi milioni 2.1. Aidha, idadi ya televisheni kwa njia ya waya imeongezeka kwa asilimia 2 kutoka televisheni 16,957 katika robo mwaka iliyoishia Septemba 2025 na kufikia televisheni 17,280.

Sekta ya posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto imeonesha uwepo wa shughuli mbalimbali ukidhihirishwa na uwepo wa masanduku ya posta na mifuko binafsi ya barua 158,073. Pia sekta hii imekua na jumla ya wateja 72,491 wa kampuni/taasisi na wateja binafsi. Katika kipindi husika, Jumla ya bidhaa za kiposta 554,261 zilitumwa ndani ya nchi na bidhaa 30,065 zilitumwa nje ya nchi. Vilevile, jumla ya bidhaa za kiposta 814,062 zilipokelewa ndani ya nchi na bidhaa 46,362 zilipokelewa kutoka nje ya nchi. Hii inaonesha umuhimu wa sekta ya posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto katika kuwaunganisha wananchi kibiashara.

# Yaliyomo


**1 Huduma za Mawasiliano ya Simu na Intaneti** **1**
1.1 Idadi ya laini za simu 2
1.2 Bei za huduma ya mawasiliano ya simu 6
1.3 Idadi ya dakika na ujumbe mfupi (SMS) kwa huduma ya mawasiliano ya simu 10
1.4 Kuzuru 17
1.5 Vifaa vya mawasiliano vinavyotumia laini za simu 18
1.6 Mgawanyo wa minara ya mawasiliano ya simu 19
1.7 Mgawanyo wa mitambo ya kurushia mawimbi ya simu 20
1.8 Ueneaji wa miundombinu ya mawasiliano 21
1.9 Huduma za intaneti 22
1.10 Huduma za pesa mtandao 31
1.11 Ubora wa huduma za simu na intaneti 33
1.12 Majaribio ya ulaghai 39
1.13 Leseni za huduma ya mawasiliano ya simu na intaneti 42
1.14 Vyeti 42

**2 Huduma za Utangazaji** **43**
2.1 Visimbuzi vilivyolipiwa angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu 44
2.2 Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya 45
2.3 Ueneaji wa huduma za utangazaji 47
2.4 Utekelezaji wa masharti ya leseni za utangazaji 48
2.5 Leseni za huduma ya utangazaji 51

**3 Huduma za Posta na Usafirishaji wa Vifurushi na Vipeto** **52**
3.1 Idadi ya masanduku ya posta 53
3.2 Wateja wa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto 53
3.3 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa 53
3.4 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa 55
3.5 Ubora wa huduma za Posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto 56
3.6 Leseni za huduma ya Posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto 57

**4 Hitimisho** **58**

# Orodha ya Maneno

| Na. | Kipengele | Maelezo |
|---|---|---|
| 1 | Usajili hai | Usajili wa laini ya simu ambapo imetumika angalau mara moja (sauti, SMS, data) katika kipindi cha siku 90 zilizopita. |
| 2 | Teknolojia ya mtandao wa simu za mkononi wa kizazi cha pili (2G) | Teknolojia ya kizazi cha pili ya mawasiliano ya simu za mkononi inayoruhusu mawasiliano ya simu ya sauti, ujumbe mfupi wa maneno na intaneti (data) yenye kasi ya kiwango cha chini. |
| 3 | Teknolojia ya mtandao wa simu za mkononi wa kizazi cha tatu (3G) | Teknolojia ya kizazi cha tatu ya mawasiliano ya simu za mkononi inayoruhusu mawasiliano ya simu ya sauti, intaneti (data) ya kasi ya wastani na video. |
| 4 | Teknolojia ya mtandao wa simu za mkononi wa kizazi cha nne (4G) | Teknolojia ya kizazi cha nne ya mawasiliano ya simu za mkononi yenye kasi ya juu ya intaneti (data) na kiwango cha chini cha ucheleweshaji na uwezo mkubwa kuliko teknolojia ya 3G. |
| 5 | Teknolojia ya mtandao wa simu za mkononi wa kizazi cha tano (5G) | Teknolojia ya kizazi cha tano ya mawasiliano ya simu za mkononi yenye kasi ya juu zaidi ya intaneti (data), kiwango cha chini sana cha ucheleweshaji na uwezo mkubwa wa kuunganisha karibu kila kitu kwa njia ya mtandao. |
| 6 | Usajili wa Intaneti yenye kasi ya juu kupitia simu za mkononi (Mobile Broadband) | Usajili wa mitandao ya intaneti yenye kasi ya juu kupitia simu za mkononi yenye kasi ya angalau 2 Mbps na kuendelea. |
| 7 | Huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto | Huduma maalum za posta kwa ajili ya ukusanyaji wa haraka, usafirishaji na uwasilishaji wa vifurushi na vipeto, tofauti na huduma za kawaida za posta. |
| 8 | Mfumo wa urushaji wa matangazo ya Televisheni wa kidijitali (DTT) | Ni mfumo wa urushaji wa matangazo ya televisheni kidijitali unaotumia miumbombinu ya mawasiliano iliyosimikwa ardhini. |
| 9 | Mfumo wa Urushaji wa Matangazo ya Televisheni kidigitali kwa njia ya Satelaiti (DTH) | Ni mfumo wa urushaji wa matangazo ya televisheni kidijitali kwa njia ya satelaiti moja kwa moja hadi nyumbani. |
| 10 | Usajili wa intaneti ya kasi ya juu isiyohamishika | Ni usajili wa intaneti yenye kasi ya juu isiyohamishika inayotumia teknolojia ya nyaya za faiba, za kawaida, satelaiti au bila kutumia waya (FWA). |
| 11 | Ueneaji wa kijiografia | Upeo na mipaka ya eneo la kijiografia ambalo huduma au mtandao fulani unapatikana na unaweza kufikiwa na watumiaji, bila kuzingatia kama huduma hiyo imesajiliwa au inatumika kwa wakati huo. |
| 12 | Uwezo wa njia ya mawasiliano ya Kimataifa | Jumla ya uwezo wa vifaa vilivyowekwa wa kusambaza data kupitia njia za kimataifa za intaneti zinazounganisha nchi na nchi nyingine duniani, unaopimwa kwa biti kwa sekunde (kama Mbps, Gbps au Tbps), bila kujali kiasi cha data kinachopitishwa kwa wakati husika. |
| 13 | Muda unaohitajika kwa paketi ya data kusafiri | Muda unaohitajika kwa paketi ya data kusafiri kutoka kwenye chanzo hadi sehemu ya kupokelewa na kurudi. |
| 14 | Mawasiliano ya Mashine kwa Mashine (M2M) | Mabadilishano ya moja kwa moja ya taarifa kati ya vifaa au mashine, bila kuingiliwa na binadamu. |
| 15 | Mawasiliano ya simu nje ya mtandao | Mawasiliano ya simu kutoka mtandao mmoja wa simu kwenda mtandao mwingine wa simu. |
| 16 | Mawasiliano ya simu ndani ya mtandao | Mawasiliano ya simu ndani ya mtandao mmoja wa simu. |
| 17 | Mtu kwa Mtu (P2P) | Mawasiliano ya pande mbili kati ya watu binafsi. |

| Na. | Kipengele | Maelezo |
|---|---|---|
| 18 | Kiwango cha matumizi (Upenyo) | Asilimia ya idadi ya watu wanaotumia huduma fulani. |
| 19 | Asilimia ya watu wanaofikiwa na huduma fulani ya mawasiliano | Asilimia ya watu katika eneo fulani ambao wanafikiwa huduma fulani ya mawasiliano. |
| 20 | Ubora wa Huduma (QoS) | Ni kiwango cha jumla cha utendaji wa huduma za mawasiliano |
| 21 | Huduma ya Kuzuru | Uwezo wa watumiaji wa huduma za simu za mkononi kutumia simu zao za mkononi (sauti, SMS, data) nje ya eneo la mtandao wao wa nyumbani. |
| 22 | Kuzuru kwenda | Maana yake ni mtumiaji wa simu ya mkononi kuunganishwa na mtandao mwingine wakati yuko nje ya eneo linalohudumiwa na mtandao wake wa nyumbani. |
| 23 | Kuzuru kutoka | Simu za wateja wageni (waliotembelea) wanaopiga na kupokea simu ndani ya nchi (inbound roaming). Maana yake ni mtumiaji wa simu ya mkononi kutoka mtandao mwingine anapotumia mtandao wako akiwa ndani ya eneo linalohudumiwa na mtandao wako. |

# Muhtasari wa takwimu za Sekta ya Mawasiliano

**Idadi ya laini za simu**

**106.9M** (156.9%)

**Utumiaji wa intaneti**

**58.1M** (85.3%)

Upenyo

**Idadi ya dakika ndani ya nchi**

**47.2B**

**Idadi ya dakika kutoka nje ya nchi**

**50.6M**

**Matumizi ya intaneti**

**808 PB**

**Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa**

**2.1M**

**17.3K**

**Televisheni kwa njia ya waya**

**Asilimia ya watu waliofikiwa na huduma ya intaneti ya kasi**

3G **93.9%**

5G **30.1%**

4G **94.2%**

**Bidhaa zilizotumwa**

554,261 — 30,065

**Bidhaa zilizopokelewa**

814,062 — 46,362

**Simu Janja**

**28.5M**

41.8%

Upenyo

# Sura ya kwanza

## Huduma za Mawasiliano ya Simu na Intaneti



# 1. Huduma za Mawasiliano ya Simu na Intaneti

Sehemu hii inawasilisha takwimu za laini ya simu, idadi ya dakika, ujumbe mfupi wa maneno (SMS), huduma ya intaneti, bei, vifaa vya mawasiliano, ubora wa huduma, pesa mtandao, majaribio ya ulaghai, miundombinu, upatikanaji wa huduma, na idadi ya watoa huduma kwa kila mwezi na robo mwaka.

## 1.1. Idadi ya laini za simu

Sehemu hii inawasilisha idadi ya laini za simu za mkononi na za mezani ambazo zilitumika kwenye huduma ya mawasiliano angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita. Kuna aina mbili za laini zinazotumika kwa mawasiliano, baina ya binadamu (Person to Person - P2P) na zinazotumika kwa mawasiliano ya vifaa na mitambo (Machine to Machine - M2M).

Jumla ya idadi ya laini (P2P na M2M) zilizosajiliwa imeongezeka kwa 7.7% kutoka milioni 99.3 katika robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2025 hadi milioni 106.9 kwa robo ya mwaka inayoishia Desemba 2025.

**Kufikia Septemba 2025** | **Kufikia Desemba 2025**

**Milioni 99.3** | **Milioni 106.9** | **7.7%**

Jedwali 1.1 linaonesha idadi ya laini za simu za mkononi na mezani zilizosajiliwa kwa robo mwaka inayoishia Desemba 2025.

**Jedwali 1.1: Idadi ya laini za simu za mkononi (P2P na M2M) na mezani**

| Mwezi | Simu za mkononi | Simu za mezani | Jumla |
|---|---|---|---|
| Oktoba | 102,222,722 | 111,369 | 102,334,091 |
| Novemba | 104,550,775 | 111,473 | 104,662,248 |
| Desemba | 106,823,601 | 111,600 | 106,935,201 |

Laini za simu zimegawanywa kwa matumizi ya watu na mashine.

### 1.1.1 Idadi ya laini za P2P

**Kielelezo 1.1.1: Idadi ya laini za P2P**



**Mpaka kufikia Desemba 2025**

**Milioni 105.8**

**Milioni 98.2**

**Mpaka kufikia Septemba 2025**

**7.8%**

Laini za simu za mkononi na mezani zilizosajiliwa kwa ajili ya P2P zimeongezeka kwa 7.8% katika robo mwaka inayoishia Desemba 2025

Idadi ya laini za simu kwa matumizi ya watu kwa robo mwaka inayoishia Desemba 2025 imeoneshwa kwenye jedwali 1.1.1.

**Jedwali 1.1.1: Idadi ya laini za simu za P2P zilizosajiliwa kwa kila mtoa huduma**

| Mwezi | Airtel | Halotel | Yas | TTCL | Vodacom | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Oktoba | 21,986,955 | 16,632,749 | 29,810,835 | 1,686,826 | 31,073,644 | 101,191,009 |
| Novemba | 22,504,187 | 16,951,842 | 30,481,470 | 1,708,125 | 31,875,246 | 103,520,870 |
| Desemba | 22,945,425 | 17,504,224 | 30,844,026 | 1,731,642 | 32,776,821 | 105,802,138 |

## 1.1.2 Idadi ya laini za simu kwa ajili ya vifaa (M2M)

**Kielelezo 1.1.2: Idadi ya laini za M2M**

Laini zilizosajiliwa kwa ajili ya mawasiliano ya M2M zimeongezeka kwa laini 2,923 kwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2025

**Mpaka kufikia Desemba 2025**

**Milioni 1.133**

**Milioni 1.130**

**Mpaka kufikia Septemba 2025**

**0.3%**

Jedwali 1.1.2 linaonesha idadi ya laini za simu kwa ajili ya matumizi ya vifaa kwa kila mtoa huduma kwa robo mwaka inayoishia Desemba 2025.

**Jedwali 1.1.2: Idadi ya laini za M2M zilizosajiliwa kwa kila mtoa huduma**

| Mwezi | Airtel | Halotel | Yas | TTCL | Vodacom | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Oktoba | 358,019 | 84,220 | 78,463 | 3,467 | 618,913 | 1,143,082 |
| Novemba | 354,310 | 85,370 | 77,938 | 3,467 | 620,293 | 1,141,378 |
| Desemba | 338,211 | 86,670 | 79,859 | 3,465 | 624,858 | 1,133,063 |

## 1.1.3 Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma


Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma kwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2025 umeoneshwa kwenye Jedwali 1.1.3.

**Jedwali 1.1.3: Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma**

| Mwezi | Airtel | Halotel | Yas | TTCL | Vodacom | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Oktoba | 22,344,974 | 16,716,969 | 29,889,298 | 1,690,293 | 31,692,557 | 102,334,091 |
| Novemba | 22,858,497 | 17,037,212 | 30,559,408 | 1,711,592 | 32,495,539 | 104,662,248 |
| Desemba | 23,283,636 | 17,590,894 | 30,923,885 | 1,735,107 | 33,401,679 | 106,935,201 |

Vodacom inaongoza kwenye soko kwa kuwa na 31.2% ikifuatiwa na Yas 28.9% na Airtel 21.8% kama inavyooneshwa kwenye chati 1.1.3.

**Chati 1.1.3: Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma**





## 1.1.4 Idadi ya laini za simu kwa kila mkoa na jinsia

**Kielelezo 1.1.4: Idadi ya laini za simu (P2P) kwa kila jinsia**




Katika robo ya mwaka inayoishia Desemba 2025, Dar es Salaam ilishika nafasi ya kwanza kwa kuwa na laini milioni 19.68, Mwanza ilishika nafasi ya pili kwa kuwa na laini milioni 7.09, Arusha ilishika nafasi ya tatu kwa kuwa na laini milioni 6.44, Mbeya ilishika nafasi ya nne ikiwa na laini milioni 6.15, na Dodoma ilishika nafasi ya tano kwa kuwa na laini milioni 5.71. Idadi ya laini za simu kwa kila mkoa imeoneshwa kwenye ramani 1.1.4.

**Ramani 1.1.4: Idadi ya laini za simu za mkononi na mezani kwa kila mkoa**




## 1.1.5 Mwenendo wa idadi ya laini za simu

Mwenendo wa idadi ya laini za simu kwa ajili ya mawasiliano ya simu kwa robo mwaka na kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita umeoneshwa katika Jedwali 1.1.5a na 1.1.5b.

**Jedwali 1.1.5a: Mwenendo wa idadi ya laini za simu kwa kipindi cha robo mwaka**

| | Machi 2025 | Juni 2025 | Septemba 2025 | Desemba 2025 |
|---|---|---|---|---|
| Laini za simu za mkononi | 90,298,941 | 92,656,179 | 99,184,621 | 106,823,601 |
| Laini za simu za mezani | 79,054 | 79,619 | 111,169 | 111,600 |
| **Jumla ya laini** | 90,377,995 | 92,735,798 | 99,295,790 | 106,935,201 |
| **Upenyo** | **132.6%** | **136.1%** | **145.7%** | **156.9%** |

**Jedwali 1.1.5b: Idadi ya laini za simu kwa miaka mitano iliyopita**

| | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Simu za mkononi | 54,044,384 | 60,192,331 | 70,215,144 | 86,769,161 | 106,823,601 |
| Simu za mezani | 71,834 | 84,696 | 75,732 | 78,299 | 111,600 |
| **Jumla** | **54,118,218** | **60,277,027** | **70,290,876** | **86,847,460** | **106,935,201** |
| **Upenyo** | **88.0%** | **98.0%** | **111.0%** | **133.5%** | **156.9%** |

## 1.2 Bei za huduma za mawasiliano ya simu

Sehemu hii inawasilisha wastani wa bei ndani na nje ya vifurushi (pamoja na kodi) kwa huduma za sauti, SMS, na data kwa matumizi ya ndani na nje ya mtandao, Afrika Mashariki (EA) na mataifa mengine (RoW).

### 1.2.1 Bei za huduma za mawasiliano ya simu nje ya kifurushi

Hizi ni bei zinazotozwa kwa huduma za sauti kwa dakika, SMS, na data kwa MB bila kujiunga katika kifurushi.

**Kielelezo 1.2.1: Bei za huduma za mawasiliano ya simu**

| | Septemba 2025 | Desemba 2025 | Badiliko |
|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 29.00 | 29.00 | 0.0% |
| Nje ya mtandao | 29.00 | 29.00 | 0.0% |
| SMS Kitaifa | 8.10 | 8.10 | 0.0% |
| SMS Kimataifa | 189.60 | 189.60 | 0.0% |
| Afrika Mashariki | 247.52 | 247.52 | 0.0% |
| Mataifa mengine | 2,315.82 | 2,315.82 | 0.0% |
| Data | 9.35 | 9.35 | 0.0% |

Kama inavyooneshwa katika muhtasari hapo juu, bei za kupiga simu ndani ya mtandao, kupiga simu nje ya mtandao, kupiga simu Afrika Mashariki, kupiga simu mataifa mengine, SMS kitaifa, SMS kimataifa na data hazikubadilika.

### 1.2.1.1 Bei za huduma ya sauti (Tsh)

Hizi ni bei za sauti kwa dakika moja kwa kupiga simu ya ndani ya nchi au ya kimataifa bila kujiunga kwenye kifurushi. Bei za huduma ya sauti kwa robo ya mwaka inayoishia Desemba 2025 kwa simu za ndani na nje ya nchi kwa kila mtoa huduma zimeoneshwa kwenye Jedwali 1.2.1.1.

**Jedwali 1.2.1.1: Bei (Tsh) za kupiga simu ndani na nje ya nchi kwa kila mtoa huduma**

| Mtoa huduma | Ndani ya mtandao | Nje ya mtandao | Afrika Mashariki | Mataifa mengine |
|---|---|---|---|---|
| Airtel | 30.00 | 30.00 | 260.00 | 2,350.00 |
| Halotel | 25.00 | 25.00 | 250.00 | 1,424.44 |
| Yas | 30.00 | 30.00 | 260.00 | 2,550.00 |
| TTCL | 30.00 | 30.00 | 217.60 | 2,871.33 |
| Vodacom | 30.00 | 30.00 | 250.00 | 2,383.33 |
| **Wastani** | 29.00 | 29.00 | 247.52 | 2,315.82 |

Jedwali 1.2.1.1 linaonesha kuwa hakuna utofauti wa gharama za kupiga simu ndani na nje ya mtandao. Wakati watoa huduma wote walitoza Tsh 30 kwa dakika ndani na nje ya mtandao, Halotel alitoza Tsh 25 kwa dakika ndani na nje ya mtandao.

Wastani wa bei ya huduma ya sauti ndani na nje ya mtandao katika robo mwaka iliyoishia Desemba ulibakia TZS 29 kama ulivyokuwa katika robo mwaka iliyoishia Septemba 2025. Aidha, Jedwali 1.2.1.1 linaonesha kuwa bei ya huduma ya sauti kimataifa zilitofautiana baina ya watoa huduma. Wastani wa bei ya huduma ya sauti kwa dakika moja kwa Afrika Mashariki na nchi nyingine ni Tsh 247.52 na 2,315.82 mtawalia.

### 1.2.1.2 Bei za SMS na data (Tsh)

Bei bila kifurushi (pamoja na kodi) nje na ndani ya nchi kwa SMS na data hadi Desemba 2025 zimeoneshwa kwenye Jedwali 1.2.1.2.

**Jedwali 1.2.1.2: Bei (Tsh) za SMS na data**

| Mtoa huduma | SMS ndani ya nchi | SMS nje ya nchi | Data/Mb |
|---|---|---|---|
| Airtel | 8.00 | 215.00 | 9.35 |
| Halotel | 6.50 | 95.00 | 9.35 |
| Yas | 8.00 | 215.00 | 9.35 |
| TTCL | 10.00 | 138.06 | 9.35 |
| Vodacom | 8.00 | 285.00 | 9.35 |
| Wastani | 8.10 | 189.60 | 9.35 |

Wastani wa bei ya kutuma SMS ndani ya nchi, kutuma SMS nje ya nchi na bei ya data kwa Desemba 2025 ulibaki kama ilivyokuwa kwenye robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2025.

### 1.2.2 Bei za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi (Tsh)

Bei za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi (pamoja na kodi) kwa dakika moja ya sauti, SMS moja na MB moja ya data kwa watumiaji waliojiunga na kifurushi zimeoneshwa kwenye jedwali 1.2.2a.

**Jedwali 1.2.2a: Bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi**

| Kipindi | Ndani ya mtandao | Nje ya mtandao | SMS | Data |
|---|---|---|---|---|
| Desemba 2025 | 5.11 | 6.33 | 1.44 | 2.06 |
| Septemba 2025 | 5.48 | 6.24 | 1.46 | 2.08 |
| Badiliko % | -6.7% | 1.5% | -1.2% | -0.7% |

Jedwali 1.2.2a linaonesha kuwa bei za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi zimebadilika kwa viwango tofauti katika robo ya mwaka inayoishia Desemba 2025 ikilinganishwa na robo ya mwaka inayoishia Septemba 2025.

Jedwali 1.2.2b linaonesha wastani wa bei za huduma za mawasiliano ya simu katika kifurushi kwa kila mtoa huduma.

**Jedwali 1.2.2b: Bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi kwa kila mtoa huduma**

| Mtoa huduma | Ndani ya mtandao | Nje ya mtandao | SMS | Data |
|---|---|---|---|---|
| Airtel | 4.39 | 7.62 | 1.19 | 2.05 |
| Halotel | 4.51 | 5.21 | 1.52 | 2.05 |
| Yas | 5.30 | 6.10 | 1.22 | 2.04 |
| TTCL | 6.80 | 6.80 | 2.07 | 2.08 |
| Vodacom | 4.55 | 5.92 | 1.22 | 2.10 |
| Wastani kwa Sekta | 5.11 | 6.33 | 1.44 | 2.06 |

### 1.2.3 Wastani wa bei za huduma za mawasiliano ya simu

Wastani wa bei za huduma za mawasiliano ya simu ndani na nje ya kifurushi kwa robo mwaka inayoishia Desemba 2025 imeoneshwa kwenye Jedwali 1.2.3.

**Jedwali 1.2.3: Wastani wa bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu**

| | Ndani ya mtandao | Nje ya mtandao | SMS | Data |
|---|---|---|---|---|
| Wastani bila kifurushi | 29.00 | 29.00 | 8.10 | 9.35 |
| Wastani katika kifurushi | 5.11 | 6.33 | 1.44 | 2.06 |

Jedwali 1.2.3 linaonesha kuwa wastani wa bei za huduma ya mawasiliano ya simu ndani ya kifurushi ni ndogo ikilinganishwa na wastani wa bei nje ya kifurushi na hivyo kusababisha watumiaji wengi (99.9%) kupendelea kujiunga na huduma za vifurushi.

### 1.2.4 Mwenendo wa wastani wa bei za huduma za mawasiliano ya simu

Mwenendo wa wastani wa bei za huduma za sauti na SMS nje ya vifurushi, kitaifa na kimataifa katika kipindi cha robo mwaka na miaka mitano imeoneshwa kwenye Jedwali 1.2.4a, 1.2.4b, 1.2.4c, 1.2.4d, 1.2.4e, 1.2.4f, 1.2.4g na 1.2.4h.

**Jedwali 1.2.4a: Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh kwa dakika) za huduma za sauti kitaifa nje ya vifurushi kwa kipindi cha robo mwaka**

| | Machi 2025 | Juni 2025 | Septemba 2025 | Desemba 2025 |
|---|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 26.00 | 26.00 | 29.00 | 29.00 |
| Nje ya mtandao | 28.00 | 28.00 | 29.00 | 29.00 |

**Jedwali 1.2.4b: Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh kwa dakika) za huduma za sauti kitaifa nje ya vifurushi kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita**

| | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 34.00 | 32.00 | 29.00 | 26.00 | 27.50 |
| Nje ya mtandao | 34.00 | 32.00 | 30.00 | 28.00 | 28.50 |

**Jedwali 1.2.4c: Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh kwa dakika) za huduma za sauti kimataifa nje ya vifurushi kwa kipindi cha robo mwaka**

| | Machi 2025 | Juni 2025 | Septemba 2025 | Desemba 2025 |
|---|---|---|---|---|
| Afrika Mashariki | 627.80 | 247.52 | 247.52 | 247.52 |
| Mataifa mengine | 1,935.00 | 2,175.15 | 2,315.82 | 2,315.82 |

**Jedwali 1.2.4d: Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh kwa dakika) za huduma za sauti kimataifa nje ya vifurushi kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita**

| | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Afrika Mashariki | 966.00 | 1,103.00 | 1,171.00 | 684.00 | 342.59 |
| Mataifa mengine | 1,564.00 | 1,817.00 | 1,776.00 | 2,055.00 | 2,185.45 |

**Jedwali 1.2.4e: Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh) za kutuma SMS kitaifa na kimataifa nje ya vifurushi kwa kipindi cha robo mwaka**

| | Machi 2025 | Juni 2025 | Septemba 2025 | Desemba 2025 |
|---|---|---|---|---|
| SMS kitaifa | 7.80 | 7.80 | 8.10 | 8.10 |
| SMS kimataifa | 189.60 | 189.60 | 189.60 | 189.60 |

**Jedwali 1.2.4f: Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh) za kutuma SMS kitaifa na kimataifa nje ya vifurushi kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita**

| | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| SMS kitaifa | 13.00 | 11.00 | 11.00 | 7.80 | 7.95 |
| SMS kimataifa | 172.00 | 193.00 | 200.00 | 189.60 | 189.60 |

**Jedwali 1.2.4g: Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi kwa kipindi cha robo mwaka**

| | Machi 2025 | Juni 2025 | Septemba 2025 | Desemba 2025 |
|---|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 4.80 | 4.80 | 5.48 | 5.11 |
| Nje ya mtandao | 6.07 | 5.96 | 6.24 | 6.33 |
| SMS | 1.55 | 1.52 | 1.46 | 1.44 |
| Data | 2.12 | 2.12 | 2.08 | 2.06 |

**Jedwali 1.2.4h: Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita**

| | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 7.84 | 7.27 | 4.90 | 4.68 | 5.05 |
| Nje ya mtandao | 8.69 | 7.78 | 6.30 | 6.22 | 6.15 |
| SMS | 3.35 | 2.69 | 1.37 | 1.46 | 1.49 |
| Data | 1.61 | 1.86 | 2.14 | 2.17 | 2.10 |

## 1.3 Idadi ya dakika na ujumbe mfupi (SMS) kwa huduma ya mawasiliano ya simu

Sehemu hii inaonesha idadi ya dakika zilizopigwa ndani na nje ya nchi pamoja na ujumbe mfupi wa maneno.

### 1.3.1 Idadi ya dakika za huduma ya sauti

#### 1.3.1.1 Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani ya nchi

Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani na nje ya mtandao ilipungua kwa 0.3% katika robo ya mwaka iliyoishia Desemba 2025 kama ilivyooneshwa kwenye kielelezo hapo chini.

| Robo mwaka iliyoishia Septemba 2025 | Robo mwaka iliyoishia Desemba 2025 | |
|---|---|---|
| **Bilioni 47.4** | **Bilioni 47.2** | **0.3%** ↓ |

Uchambuzi unaonesha kuwa, katika robo ya mwaka iliyoishia Desemba 2025 idadi ya dakika ndani mtandao iliongezeka kwa 4.8% na nje ya mtandao ilipungua kwa 5.3% kama inavyooneshwa katika Kielelezo 1.3.1.1.

**Kielelezo 1.3.1.1: Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani ya nchi**

| | Robo mwaka iliyoishia Septemba 2025 | Robo mwaka iliyoishia Desemba 2025 | Mabadiliko |
|---|---|---|---|
| Ndani ya Mtandao | 23.6 Bilioni | 24.7 Bilioni | 4.8% ▲ |
| Nje ya Mtandao | 23.8 Bilioni | 22.5 Bilioni | 5.3% ▼ |


Jedwali 1.3.1.1a linaonesha kuwa dakika bilioni 47.2 zilitumika katika robo mwaka iliyoishia Desemba 2025 ikilinganishwa na dakika bilioni 47.4 katika robo mwaka iliyoishia Septemba 2025. Katika kipindi hicho, Mwezi Oktoba 2025 ulikuwa wenye idadi ya dakika nyingi zaidi ikilinganishwa na Novemba na Desemba. Pia, mwenendo wa idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani ya nchi kwa kipindi cha robo mwaka na miaka mitano iliyopita unaoneshwa kwenye Jedwali 1.3.1.1b na 1.3.1.1c.

### Jedwali 1.3.1.1a: Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani na nje ya mtandao nchini


| | Oktoba | Novemba | Desemba | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 8,462,639,301 | 8,059,122,302 | 8,182,220,601 | **24,703,982,204** |
| Nje ya mtandao | 8,224,483,067 | 7,982,928,425 | 6,306,816,461 | **22,514,227,953** |
| **Jumla** | 16,687,122,368 | 16,042,050,727 | 14,489,037,062 | **47,218,210,157** |

Mgawanyo wa dakika ndani na nje ya mtandao nchini kwa kila mtoa huduma umeoneshwa kwenye Chati 1.3.1.1a na 1.3.1.1b. Airtel imeongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya dakika za ndani ya mtandao (35.2%) na nje ya mtandao (31.9%).

### Chati 1.3.1.1a: Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti ndani ya mtandao kwa kila mtoa huduma




### Chati 1.3.1.1b: Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti nje ya mtandao kwa kila mtoa huduma




### Jedwali 1.3.1.1b: Mwenendo wa idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani ya nchi kwa kipindi cha robo mwaka


| | Machi 2025 | Juni 2025 | Septemba 2025 | Desemba 2025 |
|---|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 20,223,164,062 | 21,492,956,952 | 23,574,844,856 | 24,703,982,204 |
| Nje ya mtandao | 20,345,309,688 | 21,759,205,362 | 23,776,107,671 | 22,514,227,953 |
| Jumla | 40,568,473,750 | 43,252,162,314 | 47,350,952,527 | 47,218,210,157 |

**Jedwali 1.3.1.1c: Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani ya nchi kwa miaka mitano iliyopita**

| | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 51,673,651,476 | 62,678,814,642 | 77,770,241,513 | 81,916,822,649 | 89,994,948,074 |
| Nje ya mtandao | 43,194,917,029 | 60,064,367,493 | 67,100,445,506 | 76,215,903,038 | 88,394,850,674 |
| Jumla | 94,868,568,505 | 122,743,182,135 | 144,870,687,019 | 158,132,725,687 | 178,389,798,748 |

## 1.3.1.2 Idadi ya dakika za huduma ya sauti nje ya nchi

Idadi ya dakika kwenda na kutoka nje ya nchi imeoneshwa hapo chini.




Kielelezo kinaonesha kuwa idadi ya dakika kwenda nje ya nchi imeongezeka kwa 5% na dakika kutoka nje ya nchi imeongezeka kwa 16%. Vilevile, takwimu zinaonesha kulikuwa na idadi kubwa ya dakika kwenda nje ya nchi ikilinganishwa na zilizotoka nje ya nchi.


Jumla ya dakika kwenda na kutoka Afrika Mashariki (EA), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na mataifa mengine (RoW) kwa robo ya mwaka iliyoishia Desemba 2025 imeoneshwa katika Jedwali 1.3.1.2a. Mwenendo wa idadi ya dakika kimataifa umeoneshwa kwenye Jedwali 1.3.1.2b na 1.3.1.2c.

**Jedwali 1.3.1.2a: Idadi ya dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka EA, SADC na RoW kwa robo mwaka inayoishia Desemba 2025**


| | Oktoba | Novemba | Desemba | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Kwenda EA | 48,418,608 | 48,569,848 | 50,916,142 | **147,904,598** |
| Kutoka EA | 14,274,338 | 15,031,571 | 13,539,230 | **42,845,139** |
| Kwenda SADC | 143,381 | 172,766 | 95,799 | **411,946** |
| Kutoka SADC | 307,880 | 398,051 | 202,289 | **908,220** |
| Kwenda RoW | 1,699,147 | 2,750,303 | 748,626 | **5,198,076** |
| Kutoka RoW | 1,933,540 | 3,332,643 | 1,547,368 | **6,813,551** |

Mgawanyo wa dakika kwenda na kutoka EA, SADC na Mataifa Mengine (RoW) umeoneshwa kwenye Chati 1.3.1.2a , Chati 1.3.1.2b na Chati 1.3.1.2c.


**Chati 1.3.1.2a: Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka EA**




**Chati 1.3.1.2b: Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka SADC**




**Chati 1.3.1.2c: Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka RoW**




**Jedwali 1.3.1.2b: Idadi ya dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka EA, SADC na RoW kwa robo mwaka**

| | Machi 2025 | Juni 2025 | Septemba 2025 | Desember 2025 |
|---|---|---|---|---|
| Kwenda EA | 129,398,936 | 156,913,941 | 143,487,145 | 147,904,598 |
| Kutoka EA | 31,009,232 | 34,761,058 | 39,343,813 | 42,845,139 |
| Kwenda SADC | 281,939 | 310,606 | 270,090 | 411,946 |
| Kutoka SADC | 591,422 | 835,650 | 618,503 | 908,220 |
| Kwenda RoW | 3,715,324 | 2,224,864 | 2,410,516 | 5,198,076 |
| Kutoka RoW | 5,023,166 | 4,155,135 | 3,466,597 | 6,813,551 |

**Jedwali 1.3.1.2c: Idadi ya dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka EA na RoW kwa miaka mitano iliyopita**

| | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kwenda EA | 9,097,165 | 8,927,113 | 95,473,684 | 363,293,881 | 577,704,620 |
| Kutoka EA | 15,853,362 | 13,594,473 | 34,994,641 | 108,663,455 | 147,959,242 |
| Kwenda RoW | 24,856,947 | 26,034,131 | 19,510,999 | 36,294,294 | 14,823,361 |
| Kutoka RoW | 49,885,142 | 33,374,619 | 23,681,940 | 24,858,074 | 22,412,244 |

## 1.3.2 Idadi ya ujumbe mfupi wa maneno (SMS)

### 1.3.2.1 Idadi ya SMS ndani ya nchi

Kielelezo kinaonesha idadi ya SMS imeongezeka kwa 9.2% kwa robo ya mwaka inayoishia Desemba 2025.

| Robo mwaka inayoishia Septemba 2025 | Robo mwaka inayoishia Desemba 2025 | |
|---|---|---|
| **Bilioni 52.9** | **Bilioni 57.8** | **9.2%** |

| Robo mwaka | SMS ndani ya mtandao | SMS nje ya mtandao | Jumla |
|---|---|---|---|
| Desemba 2025 | Bilioni 24.20 | Bilioni 33.61 | Bilioni 57.80 |
| Septemba 2025 | Bilioni 22.29 | Bilioni 30.65 | Bilioni 52.94 |
| **Badiliko** | **8.55%** | **9.64%** | **9.18%** |

Jedwali 1.3.2.1a linaonesha mabadiliko ya idadi ya SMS ndani na nje ya mtandao kwa robo mwaka inayoishia Desemba 2025. Mwezi Desemba 2025 ulikuwa na idadi kubwa ya SMS ikilinganishwa na Oktoba na Novemba.

**Jedwali 1.3.2.1a: Idadi ya SMS ndani ya nchi**

| | Oktoba | Novemba | Desemba | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 7,901,648,485 | 7,787,040,686 | 8,506,354,531 | **24,195,043,702** |
| Nje ya mtandao | 10,786,432,503 | 10,632,793,182 | 12,190,198,323 | **33,609,424,008** |
| Jumla | 18,688,080,988 | 18,419,833,868 | 20,696,552,854 | **57,804,467,710** |

Mwenendo wa idadi ya SMS ndani ya nchi imeoneshwa katika jedwali 1.3.2.1b na 1.3.2.1c.

**Jedwali 1.3.2.1b: Mwenendo wa idadi ya SMS za ndani ya nchi kwa kipindi cha robo mwaka**

| | Machi 2025 | Juni 2025 | Septemba 2025 | Desemba 2025 |
|---|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 21,081,683,531 | 22,301,400,244 | 22,288,636,639 | 24,195,043,702 |
| Nje ya mtandao | 28,937,308,450 | 30,516,070,406 | 30,654,884,978 | 33,609,424,008 |
| Jumla | 50,018,991,981 | 52,817,470,650 | 52,943,521,617 | 57,804,467,710 |

**Jedwali 1.3.2.1c: Idadi ya SMS za ndani ya nchi kwa miaka mitano iliyopita**

| | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 58,875,779,663 | 65,358,270,089 | 84,818,793,761 | 84,909,556,665 | 89,866,764,116 |
| Nje ya mtandao | 78,200,512,436 | 88,154,239,625 | 121,727,776,013 | 116,828,465,147 | 123,717,687,842 |
| Jumla | 137,076,292,099 | 153,512,509,714 | 206,546,569,774 | 201,738,021,812 | 213,584,451,958 |

## 1.3.2.2 Idadi ya SMS kutoka na kwenda nje ya nchi


Idadi ya SMS kutoka na kwenda EA, SADC na RoW imeoneshwa kwenye Jedwali 1.3.2.2a.

**Jedwali 1.3.2.2a: Idadi ya SMS kutoka na kwenda EA, SADC na RoW**


| | Oktoba | Novemba | Desemba | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Kwenda EA | 219,649 | 98,259 | 71,090 | **388,998** |
| Kutoka EA | 209,917 | 197,295 | 194,308 | **601,520** |
| Kwenda SADC | 61,678 | 50,671 | 29,744 | **142,093** |
| Kutoka SADC | 133,642 | 146,473 | 127,335 | **407,450** |
| Kwenda RoW | 467,512 | 564,851 | 486,293 | **1,518,656** |
| Kutoka RoW | 620,344 | 693,828 | 719,793 | **2,033,965** |

Jedwali 1.3.3.2a linaonesha kuwa idadi kubwa ya SMS zilipokelewa kutoka EA, SADC na RoW kuliko zilizotumwa EA, SADC na RoW. Uwiano wa SMS zilizotumwa na kupokelewa imeoneshwa kwenye Chati 1.3.2.2a, 1.3.2.2b na 1.3.2.2c.


**Chati 1.3.2.2a: Mgawanyo wa SMS kwenda na kutoka EA**




**Chati 1.3.2.2b: Mgawanyo wa SMS kwenda na kutoka SADC**



**Chati 1.3.2.2c: Mgawanyo wa SMS kwenda na kutoka RoW**




Mwenendo wa idadi ya SMS EA, SADC na RoW kwa robo mwaka na kipindi cha miaka mitano iliyopita imeoneshwa kwenye Jedwali 1.3.2.2b na 1.3.2.2c.

### Jedwali 1.3.2.2b: Idadi ya SMS kwenda na kutoka EA, SADC na RoW kwa robo mwaka

| | Machi 2025 | Juni 2025 | Septemba 2025 | Desemba 2025 |
|---|---|---|---|---|
| Kwenda EA | 435,676 | 427,754 | 461,683 | 388,998 |
| Kutoka EA | 7,835,696 | 10,495,680 | 11,533,796 | 601,520 |
| Kwenda SADC | 89,400 | 85,843 | 102,830 | 142,093 |
| Kutoka SADC | 1,033,306 | 952,425 | 902,391 | 407,450 |
| Kwenda RoW | 1,256,169 | 1,128,292 | 1,334,976 | 1,518,656 |
| Kutoka RoW | 1,785,739,892 | 2,118,318,349 | 2,667,331,794 | 2,033,965 |

### Jedwali 1.3.2.2c: Idadi ya SMS kwenda na kutoka EA na RoW kwa miaka mitano iliyopita

| | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kwenda EA | 1,425,624 | 1,700,525 | 2,233,288 | 1,896,295 | 1,714,111 |
| Kutoka EA | 89,717,530 | 58,344,672 | 37,592,410 | 41,662,728 | 30,466,692 |
| Kwenda RoW | 3,191,041 | 3,574,956 | 5,448,764 | 13,342,306 | 5,658,259 |
| Kutoka RoW | 4,599,468,894 | 4,664,200,079 | 5,562,047,440 | 5,798,188,788 | 6,576,719,572 |

## 1.4 Kuzuru

Sehemu hii inaonesha idadi ya dakika ya huduma ya sauti, SMS na Data kutoka na kwenda EA, SADC na RoW kwa huduma za kuzuru (roaming) kwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2025.

**Kielelezo 1.4: Kuzuru**

| | Dakika | SMS | Data |
|---|---|---|---|
| Kuzuru kwenda | Bilioni 7.06 | Milioni 8.11 | 7,607 PB |
| Kuzuru Kutoka | Bilioni 1.16 | Milioni 6.14 | 131,935 PB |

### 1.4.1 Kuzuru huduma ya sauti (dakika)

Idadi ya dakika kwa huduma ya kuzuru ya sauti kutoka na kwenda EA, SADC na RoW kwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2025 imeoneshwa kwenye jedwali 1.4.1.

**Jedwali 1.4.1: Kuzuru huduma ya sauti (dakika)**

| | EA | SADC | RoW | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Kuzuru kwenda | 17,002,715 | 21,631 | 7,038,200,169 | 7,055,224,515 |
| Kuzuru Kutoka | 874,566,509 | 6,027,238 | 278,930,774 | 1,159,524,521 |

### 1.4.2 Kuzuru huduma ya SMS

Idadi ya SMS kutoka na kwenda EA, SADC na RoW kwa huduma za kuzuru kwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2025 imeoneshwa kwenye jedwali 1.4.2.

**Jedwali 1.4.2: Kuzuru huduma ya SMS**

| | EA | SADC | RoW | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Kuzuru kwenda | 4,630,924 | 527,201 | 2,951,118 | 8,109,243 |
| Kuzuru Kutoka | 3,297,883 | 388,041 | 2,450,468 | 6,136,392 |

### 1.4.3 Kuzuru huduma ya intaneti

Idadi ya megabaiti kutoka na kwenda EA, SADC na RoW kwa huduma za kuzuru kwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2025 imeoneshwa kwenye jedwali 1.4.3.


**Jedwali 1.4.3: Kuzuru huduma ya intaneti (megabytes)**

| | EA | SADC | RoW | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Kuzuru kwenda | 2,097,239 | 971,469 | 7,606,624,675,161 | 7,606,627,743,869 |
| Kuzuru Kutoka | 3,748,258,883,062 | 4,675,545,411,659 | 123,511,057,949,233 | 131,934,862,243,954 |

## 1.5 Vifaa vya mawasiliano vinavyotumia laini za simu

Vifaa vya mawasiliano vinavyotumia laini ya simu ndiyo kichocheo kikubwa katika kukuza matumizi ya huduma za mawasiliano ya simu/TEHAMA nchini. Idadi ya vifaa vilivyounganishwa kwenye mitandao ya simu imeoneshwa kwenye Jedwali 1.5.

**Kielelezo 1.5: Upenyo wa simu za mkononi**




Kufikia Desemba 2025, asilimia ya upenyo wa simu janja (smartphones) kwa idadi ya watu imeongezeka kufikia 41.82% kutoka 39.53% katika mwezi Septemba 2025. Aidha, asilimia ya upenyo wa simu za rununu (feature phones) imeongezeka kutoka 86.35% mwezi Septemba 2025 na kufikia 87.11% mwezi Desemba 2025. Ueneaji wa vifaa vingine vya mawasiliano miongoni mwa watu ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 1.5.

**Jedwali 1.5: Vifaa vya mawasiliano vinavyotumia laini za simu na kuunganishwa kwenye mtandao**


| Aina ya kifaa | Idadi ya Vifaa | Upenyo (Penetration) |
|---|---|---|
| Simu za rununu (Feature phones) | 59,365,445 | 87.11% |
| Simu janja (Smartphones) | 28,500,227 | 41.82% |
| Handheld | 1,477,744 | 2.17% |
| Modem | 758,878 | 1.11% |
| Tablet | 537,853 | 0.79% |
| WLAN Router | 474,816 | 0.70% |
| IoT Device | 178,998 | 0.26% |
| Module | 87,109 | 0.13% |
| Dongle | 82,709 | 0.12% |
| Portable(include PDA) | 62,935 | 0.09% |
| Connected Computer | 13,926 | 0.02% |
| VehicleWearable | 12,376 | 0.02% |
| WearableVehicle | 7,800 | 0.01% |
| Device for the Automatic Processing of Data (APD) | 4,409 | 0.01% |

Upenyaji mdogo wa simu janja ukilinganishwa na ueneaji wa miundombinu ya mawasiliano ni fursa ya uwekezaji katika uzalishaji, uagizaji na usambazaji wa simu janja na vifaa vingine vya mawasiliano vinavyotumia laini za simu.

## 1.6 Mgawanyo wa minara ya mawasiliano ya simu

Hadi kufikia Desemba 2025, idadi ya minara ya huduma ya mawasiliano ya simu ilikuwa ni 10,029. Mkoa wa Dar es Salaam uliongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya minara 1,232. Mgawanyo wa idadi ya minara kwa kila mkoa imeoneshwa kwenye ramani 1.6.

**Ramani 1.6: Mgawanyo wa minara ya mawasiliano ya simu**




## 1.7 Mgawanyo wa mitambo ya kurushia mawimbi ya simu

Jedwali 1.7 linaonesha idadi ya mitambo ya 2G, 3G, 4G na 5G kwa kila mkoa hadi kufikia Desemba 2025.

### Jedwali 1.7: Mgawanyo wa mitambo ya kurushia mawimbi ya simu kimkoa

| Mkoa | Idadi ya mitambo ya kurushia mawimbi | | | |
|---|---|---|---|---|
| | BTS (2G) | NodeB (3G) | eNB (4G) | gNB (5G) |
| **Tanzania Bara** | | | | |
| Arusha | 746 | 706 | 714 | 53 |
| Dar-es-salaam | 2406 | 2429 | 2500 | 817 |
| Dodoma | 749 | 630 | 701 | 67 |
| Geita | 426 | 399 | 408 | 8 |
| Iringa | 424 | 381 | 403 | 7 |
| Kagera | 551 | 518 | 507 | 2 |
| Katavi | 176 | 156 | 158 | 2 |
| Kigoma | 501 | 467 | 470 | 5 |
| Kilimanjaro | 588 | 550 | 560 | 12 |
| Lindi | 376 | 289 | 320 | 3 |
| Manyara | 380 | 303 | 326 | 1 |
| Mara | 437 | 402 | 409 | 5 |
| Mbeya | 610 | 585 | 606 | 24 |
| Morogoro | 778 | 679 | 744 | 20 |
| Mtwara | 454 | 373 | 391 | 2 |
| Mwanza | 776 | 754 | 759 | 52 |
| Njombe | 338 | 284 | 303 | 3 |
| Pwani | 570 | 494 | 543 | 18 |
| Rukwa | 297 | 265 | 258 | 1 |
| Ruvuma | 457 | 364 | 380 | 4 |
| Shinyanga | 405 | 387 | 388 | 9 |
| Simiyu | 309 | 277 | 277 | 2 |
| Singida | 381 | 338 | 343 | 4 |
| Songwe | 257 | 229 | 229 | 14 |
| Tabora | 580 | 522 | 518 | 8 |
| Tanga | 659 | 566 | 585 | 11 |
| **Zanzibar** | | | | |
| Kaskazini Pemba | 65 | 63 | 57 | 2 |
| Kaskazini Unguja | 91 | 91 | 90 | 4 |
| Kusini Pemba | 67 | 68 | 66 | 2 |
| Kusini Unguja | 109 | 105 | 108 | 6 |
| Mjini Magharibi | 253 | 268 | 272 | 68 |
| **Jumla** | **15,216** | **13,942** | **14,393** | **1,255** |

**Kielelezo 1.7: Mgawanyo wa mitambo ya kurushia mawimbi kwa teknolojia**




Jedwali 1.7 linaonesha kuenea kwa kiasi kikubwa kwa teknolojia ya 2G, 3G na 4G, ikiwa na BTS 15,216, NodeB 13,942 na eNB 14,393. Aidha, gNB zimeongezeka kwa kiasi cha asilimia 19 zikiwa zimefika 1,255 na zimeenea zaidi katika maeneo ya mijini kama vile Dar es Salaam na Mjini Magharibi. Dar es Salaam inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya mitambo ya kurushia mawimbi ya mawasiliano kwa teknolojia zote (2G, 3G, 4G na 5G), na kuifanya kuwa kitovu cha mawasiliano nchini.

## 1.8 Ueneaji wa miundombinu ya mawasiliano

Uwekezaji katika miundombinu ya mawasiliano umeongeza usambaaji wa huduma ya mawasiliano kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 1.8.

**Jedwali 1.8: Ueneaji wa miundombinu ya mawasiliano**

| | | Septemba 2025 | Desemba 2025 |
|---|---|---|---|
| Asilimia ya watu waliofikiwa na huduma ya mawasiliano | 2G | 98.6% | 98.6% |
| | 3G | 93.8% | 93.9% |
| | 4G | 94.2% | 94.2% |
| | 5G | 28.9% | 30.1% |
| Asilimia ya eneo lilofikiwa na huduma ya mawasiliano | 2G | 78.2% | 79.5% |
| | 3G | 75.9% | 76.2% |
| | 4G | 76.9% | 77.3% |
| | 5G | 8.6% | 10.5% |

Jedwali 1.8, linaonesha kuenea kwa wigo wa mawasiliano 2G, 3G, 4G na 5G kufikia 98.6%, 93.9%, 94.2%, na 30.1% ya watu nchini, mtawalia. Aidha, asilimia ya eneo lilofikiwa na mawasiliano ya 2G, 3G, 4G na 5G ni 79.5%, 76.2%, 77.3%, na 10.5%, mtawalia.

## 1.9 Huduma za Intaneti

### 1.9.1 Utumiaji wa Intaneti

Huduma ya Intaneti inatolewa kwa kutumia laini za simu, waya (faiba), na mawimbi (wireless). Idadi ya utumiaji wa intaneti inatokana na laini/waya ambazo zimetumia huduma ya Intaneti angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita, bila kujali teknolojia iliyotumika (FTTX, 2G - GPRS na EDGE, 3G, 4G, au 5G).

Utumiaji wa Intaneti kwa robo ya mwaka iliyoishia Desemba 2025 imeoneshwa kwenye kielelezo hapo chini.

| Kufikia Septemba 2025 | Kufikia Desemba 2025 | |
|---|---|---|
| **Milioni 56.3** | **Milioni 58.1** | **3.2%** ↑ |

Idadi ya utumiaji wa Intaneti imeongezeka kwa 3.2% kutoka milioni 56.3 kwa robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2025 hadi milioni 58.1 kwa robo ya mwaka iliyoishia Desemba 2025.

Idadi ya utumiaji wa Intaneti kwa robo ya mwaka iliyoishia Desemba 2025 imeoneshwa kwenye Jedwali 1.9.1a. Jedwali hilo linaonesha kuwa huduma ya Intaneti kwa njia ya simu ya mkononi inapendelewa zaidi (99%) ikilinganishwa na huduma ya Intaneti isiyohamishika.

**Jedwali 1.9.1a: Idadi ya utumiaji wa Intaneti kufikia mwisho wa kila mwezi katika robo ya mwaka inayoishia Desemba 2025**


| Mwezi | Mobile Wireless | Fixed Wireless | Fixed Wired | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Oktoba | 56,250,272 | 220,217 | 135,302 | **56,605,791** |
| Novemba | 57,012,704 | 253,797 | 137,367 | **57,403,868** |
| Desemba | 57,691,394 | 275,553 | 139,317 | **58,106,264** |
| **Upenyo** | | | | **85.3%** |


Kielelezo 1.9.1a kinaonesha kuwa Intaneti ya kasi kwa huduma ya simu ndiyo njia inayopendelewa zaidi kupata Intaneti, ikiwa na laini 32,738,489 . Teknolojia ya 2G bado ina matumizi makubwa, ikiwa na laini 24,952,905. Teknolojia za faiba Nyumbani (Fiber to the Home - FTTH) na faiba Ofisini (Fiber to the Office - FTTO) zina idadi ndogo ya laini 123,052 na 16,265 mtawalia.

## Jedwali 1.9.1b: Idadi ya utumiaji wa Intaneti kwa teknolojia


| Teknolojia | Oktoba | Novemba | Desemba |
|---|---|---|---|
| 2G | 24,611,408 | 24,833,851 | 24,952,905 |
| 3G | 4,673,989 | 4,591,430 | 4,490,438 |
| 4G | 25,322,137 | 25,863,318 | 26,424,850 |
| 5G | 1,642,738 | 1,724,105 | 1,823,201 |
| FTTH | 119,658 | 121,516 | 123,052 |
| FTTO | 15,644 | 15,851 | 16,265 |
| Terrestrial fixed wireless | 212,738 | 246,278 | 267,951 |
| Setelaite | 1,866 | 1,887 | 1,950 |
| Teknolojia nyingine | 5,613 | 5,632 | 5,652 |
| **Jumla** | **56,605,791** | **57,403,868** | **58,106,264** |

**Kielelezo 1.9.1a: Utumiaji wa Intaneti kwa teknolojia**




## Chati 1.9.1a: Mgawanyo wa huduma ya Intaneti kwa njia ya simu kwa kila mtoa huduma kwa robo mwaka inayoishia Desemba 2025




## Chati 1.9.1b: Idadi ya laini za intaneti (fixed) kwa kila mtoa huduma





Usajili wa laini za Intaneti (fixed) kwa watu binafsi ni 324,339

Usajili wa laini za Intaneti (fixed) kwa Taasisi ni **90,531**

**Jedwali 1.9.1c: Idadi ya usajili kulingana na kasi ya Intaneti (Internet subscription by speed)**


| Kasi | Idadi ya usajili |
|---|---|
| <256 Kbps | 7 |
| >= 256 Kbps< 2Mbps | 1,207 |
| >= 2Mbps< 10Mbps | 26,174 |
| >= 10Mbps< 100Mbps | 380,927 |
| >= 100Mbps< 1Gbps | 6,183 |
| >= 1Gbps | 372 |
| **Jumla** | **414,870** |

**Kielelezo 1.9.1b: Mwenendo wa idadi ya utumiaji wa huduma ya Intaneti kwa robo mwaka**





Kielelezo 1.9.1b inaonesha wastani wa ukuaji wa 5.6% ya idadi ya utumiaji wa huduma ya Intaneti kutoka Machi 2025 mpaka Desemba 2025.

**Chati 1.9.1c: Mwenendo wa idadi ya laini zinazotumia huduma ya Intaneti kwa miaka mitano iliyopita**



### 1.9.2 Matumizi ya huduma ya Intaneti

Matumizi ya huduma ya Intaneti huhesabiwa kama kiasi cha data (katika Petabytes) kilichotumiwa katika kipindi husika. (1 Petabyte = $1000^3$ Megabytes). Matumizi ya huduma ya Intaneti ni kama yanavyooneka hapo chini.




**Jedwali 1.9.2a: Kiasi cha data kilichotumika katika robo ya mwaka inayoishia Desemba 2025**

| | Oktoba | Novemba | Desemba |
|---|---|---|---|
| GB | 84,291,834 | 82,458,928 | 95,058,442 |
| usajili wa intaneti | 56,250,272 | 57,012,704 | 57,691,394 |
| GB kwa kila usajili | 1.5 | 1.4 | 1.6 |

Jedwali 1.9.2 linaonesha kuwa kila usajili wa Intaneti ulitumia wastani wa GB 1.6 kwa mwezi Desemba ambayo ni pungufu ikilinganishwa na Oktoba na Novemba.

**Jedwali 1.9.2b: Kiasi cha utumiaji wa data kwa teknolojia ya Intaneti isiyohamishika katika robo ya mwaka inayoishia Desemba 2025**

| | Oktoba | Novemba | Desemba |
|---|---|---|---|
| Kiasi cha data (GB) | 176,409,394 | 174,104,864 | 196,025,156 |
| usajili wa intaneti | 355,519 | 391,164 | 414,870 |

Ongezeko la utumiaji wa intaneti unaoonekana na matumizi ya data linatoa fursa ya uwekezaji katika ujenzi wa miundombinu ya intaneti ya kasi na huduma za kidijiti.

## 1.9.3 Wastani wa kasi na ukawiaji wa intaneti

**Kielelezo 1.9.3: Wastani wa kasi ya kupakua na kupakia**

| Fixed Broadband | Kupakua (Mbps) | Kupakia (Mbps) | Ukawiaji (ms) |
|---|---|---|---|
| | 27.9 | 21.0 | 16.6 |

**1.9.3a: Kiashiria cha ubora wa huduma ya intaneti wa kupakua (Mbps) kwa maeneo yaliopimwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2025**

| Eneo la upimaji | Airtel | Halotel | Yas | TTCL | Vodacom | Wastani |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Arusha | 24.3 | 17.7 | 32.7 | 27.3 | 33.8 | 27.18 |
| Ilala | 40.1 | 17.0 | 50.3 | 26.2 | 51.8 | 37.07 |
| Kigamboni | 31.0 | 15.2 | 39.3 | 19.3 | 41.6 | 29.26 |
| Temeke | 40.0 | 18.6 | 55.6 | 23.8 | 24.8 | 32.54 |
| Kinondoni | 39.3 | 21.8 | 67.2 | 16.2 | 52.4 | 39.38 |
| Ubungo | 35.6 | 18.8 | 53.8 | 19.9 | 48.3 | 35.30 |
| Geita | 34.8 | 23.7 | 33.8 | 26.6 | 47.3 | 33.24 |
| Kagera | 32.0 | 25.0 | 30.5 | 31.0 | 40.4 | 31.79 |
| Kigoma | 25.2 | 21.2 | 32.7 | 22.5 | 20.2 | 24.38 |
| Kilimanjaro | 24.6 | 18.9 | 51.6 | 25.4 | 26.6 | 29.44 |
| Manyara | 22.8 | 19.3 | 42.2 | 22.4 | 24.2 | 26.17 |
| Mbeya | 20.2 | - | 34.5 | - | 47.1 | 33.95 |
| Pwani | 29.6 | 22.4 | 40.4 | 24.0 | 22.3 | 27.72 |
| Rukwa | 26.5 | 22.7 | 33.4 | 24.5 | 16.7 | 24.76 |
| Singida | 22.7 | 21.1 | 44.2 | 26.2 | 27.4 | 28.32 |
| Songwe | 27.6 | - | 40.5 | - | 36.6 | 34.89 |
| Tabora | 23.9 | 22.9 | 38.6 | 24.2 | 21.4 | 26.21 |
| Unguja | 13.4 | 14.9 | 40.2 | 23.4 | 27.5 | 23.88 |
| **Wastani wa Sekta** | | | | | | **30.3** |

**1.9.3b: Kiashiria cha ubora wa huduma ya intaneti kwa ukawiaji (ms) kwa maeneo yaliopimwa kwenye robo mwaka iliyoishia Desemba 2025**

| Eneo la upimaji | Airtel | Halotel | Yas | TTCL | Vodacom | Wastani |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Arusha | 41.9 | 64.9 | 94.0 | 110.7 | 50.6 | 72.40 |
| Ilala | 39.2 | 57.4 | 70.4 | 96.7 | 35.7 | 59.85 |
| Kigamboni | 44.7 | 50.7 | 78.5 | 106.4 | 41.1 | 64.28 |
| Temeke | 41.9 | 68.5 | 74.9 | 102.6 | 42.8 | 66.12 |
| Kinondoni | 49.7 | 46.5 | 67.4 | 119.5 | 36.1 | 63.83 |
| Ubungo | 53.4 | 57.3 | 75.4 | 101.0 | 39.8 | 65.39 |
| Geita | 92.7 | 48.7 | 135.7 | 129.8 | 65.5 | 94.45 |
| Kagera | 59.9 | 55.3 | 113.8 | 116.7 | 52.7 | 79.64 |
| Kigoma | 71.6 | 68.5 | 142.9 | 151.4 | 60.3 | 98.93 |
| Kilimanjaro | 36.9 | 63.7 | 63.8 | 101.7 | 50.8 | 63.38 |
| Manyara | 49.1 | 47.0 | 92.9 | 105.3 | 50.4 | 68.94 |
| Mbeya | 62.9 | - | 97.5 | - | 48.0 | 69.47 |
| Pwani | 44.1 | 43.6 | 70.0 | 97.6 | 42.6 | 59.58 |
| Rukwa | 70.5 | 69.4 | 134.5 | 119.1 | 67.1 | 92.10 |
| Singida | 55.0 | 64.1 | 93.4 | 110.5 | 48.0 | 74.17 |
| Songwe | 58.3 | - | 92.7 | - | 48.2 | 66.42 |
| Tabora | 60.7 | 61.2 | 112.3 | 123.3 | 56.2 | 82.76 |
| Unguja | 72.0 | 70.1 | 43.8 | 96.5 | 53.0 | 67.07 |
| **Wastani wa Sekta** | | | | | | **72.71** |

**1.9.3c: Kiashiria cha ubora wa upatikanaji wa huduma ya mtandao kwa maeneo yaliopimwa kwenye robo mwaka iliyoishia Desemba 2025**

| Eneo la upimaji | Airtel | Halotel | Yas | TTCL | Vodacom | Wastani |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Arusha | 99.5 | 99.8 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 99.83 |
| Ilala | - | 100.0 | 99.9 | - | 99.9 | 99.94 |
| Kigamboni | 99.9 | 99.8 | 99.9 | 99.9 | 100.0 | 99.90 |
| Temeke | 100.0 | 100.0 | 99.9 | 99.9 | 100.0 | 99.94 |
| Kinondoni | 100.0 | 100.0 | 99.9 | 100.0 | 100.0 | 99.96 |
| Ubungo | 99.9 | 100.0 | 99.9 | 99.9 | 100.0 | 99.94 |
| Geita | 99.6 | 99.9 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 99.89 |
| Kagera | 99.6 | 99.9 | 99.9 | 100.0 | 99.7 | 99.83 |
| Kigoma | 99.7 | 99.8 | 100.0 | 100.0 | 99.8 | 99.86 |
| Kilimanjaro | 99.9 | 99.6 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 99.87 |
| Manyara | 99.4 | 99.8 | 99.9 | 100.0 | 99.9 | 99.79 |
| Mbeya | 99.3 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 99.85 |
| Pwani | 99.9 | 100.0 | 99.9 | 99.9 | 99.9 | 99.92 |
| Rukwa | 99.6 | 100.0 | 99.9 | 100.0 | 100.0 | 99.90 |
| Singida | 99.9 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 99.95 |
| Songwe | 99.1 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 99.9 | 99.80 |
| Tabora | 99.8 | 99.7 | 99.9 | 100.0 | 99.9 | 99.84 |
| Unguja | 99.7 | 99.1 | 99.9 | 99.8 | 99.6 | 99.61 |
| **Wastani wa Sekta** | | | | | | **99.87** |

### 1.9.4 Uwezo wa kiunganishi cha Intaneti kimataifa

Uwezo wa kuunganisha huduma ya Intaneti kwenda nje na kuja ndani ya nchi (International Internet link capacity) unakuza matumizi ya Intaneti ndani na nje ya nchi. Jedwali 1.9.4 linaonesha kuwa nchi ina uwezo wa 14,727 Gbps kwa ajili ya uunganishaji mpya wa huduma ya Intaneti. Hii inamaanisha ni asilimia 16.3 pekee ya uwezo wa viunganisho vya kimataifa ambao umetumika.

**Jedwali 1.9.4: Uwezo wa kiunganishi cha huduma ya Intaneti kufikia Desemba 2025**

| | Uwezo unaotoka (Gbps) | Uwezo unaoingia (Gbps) |
|---|---|---|
| Jumla ya uwezo uliopo | 17,590 | 17,590 |
| Jumla ya uwezo uliotumika | 2,863 | 2,863 |
| Uwezo unaopatikana kwa uunganishaji mpya | 14,727 | 14,727 |

Pengo kati ya uwezo uliopo na uliotumika wa kiunganishi cha intaneti kimataifa linatoa fursa ya uwekezaji katika huduma ya intaneti ya kasi.

### 1.9.5 Idadi ya vikoa vya intaneti

Jumla ya idadi ya vikoa vilivyosajiliwa iliongezeka kutoka 35,621 mwishoni mwa Septemba 2025 hadi 36,223 mwishoni mwa Desemba 2025, kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 1.9.5.

**Jedwali 1.9.5: Idadi ya vikoa vya intaneti**

| Kikoa | Septemba 2025 | Desemba 2025 |
|---|---|---|
| co.tz | 27,928 | 28,379 |
| or.tz | 2,865 | 2,894 |
| ac.tz | 1,210 | 1,249 |
| go.tz | 937 | 947 |
| .tz | 2,331 | 2,409 |
| sc.tz | 285 | 284 |
| ne.tz | 30 | 25 |
| me.tz | 17 | 18 |
| info.tz | 5 | 6 |
| hotel.tz | 3 | 2 |
| mobi.tz | 3 | 3 |
| tv.tz | 3 | 3 |
| mil.tz | 4 | 4 |
| Jumla | 35,621 | 36,223 |


# 1.10 Huduma za Pesa Mtandao

Sehemu hii inawasilisha takwimu za huduma za pesa mtandao kupitia simu za mkononi zinazotolewa na watoa huduma za pesa mitandao (Mobile Money Operators) kulingana na idadi ya akaunti za pesa mtandao na miamala.

## 1.10.1 Akaunti za pesa mtandao

Idadi ya akaunti za pesa mtandao ambazo zilitumika angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita iliongezeka kwa asilimia 6.7 kutoka akaunti milioni 71.7 katika robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2025 hadi milioni 76.5 katika robo ya mwaka iliyoishia Desemba 2025.

**Kielelezo 1.10.1: Akaunti za pesa mtandao**





**Jedwali 1.10.1: Idadi ya akaunti za pesa mtandao**

| | Oktoba | Novemba | Desemba |
|---|---|---|---|
| Airtel Money | 13,495,550 | 13,815,818 | 14,180,725 |
| Azam Pesa | 47,878 | 48,619 | 47,749 |
| HaloPesa | 7,365,040 | 7,520,864 | 7,638,570 |
| Mixx by Yas | 21,928,551 | 22,278,213 | 22,592,840 |
| T- Pesa | 518,650 | 518,650 | 518,650 |
| M-pesa | 29,422,162 | 30,189,566 | 31,488,157 |
| **Jumla** | **72,777,831** | **74,371,730** | **76,466,691** |

Jedwali 1.10.1 linaonesha kuwa akaunti za pesa mtandao ziliongezeka kwa wastani wa asilimia 2.5 kwa mwezi katika robo mwaka iliyoishia Desemba 2025. Mgawanyo wa akaunti za pesa mtandao imeoneshwa kwenye Chati 1.10.1.

**Chati 1.10.1: Mgawanyo wa akaunti za pesa mtandao**



Chati 1.10.1 inaonesha kuwa soko la pesa mtandao lina ushindani, huku M-pesa ikiongoza kwa kuwa na asilimia 41.2

## 1.10.2 Idadi ya miamala ya pesa mtandao

Idadi ya miamala ya pesa mtandao kwa akaunti zilizoweka na kutuma pesa kwa njia ya pesa mtandao katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita ya robo ya mwaka iliyoishia Desemba 2025 imeoneshwa kwenye Jedwali 1.10.2a. Pia, mwenendo wa idadi ya miamala na akaunti kwa robo mwaka na miaka mitano iliyopita imeoneshwa kwenye jedwali 1.10.2b na 1.10.2c.

### Jedwali 1.10.2a: Idadi ya miamala ya pesa mtandao

| | Oktoba | Novemba | Desemba |
|---|---|---|---|
| Airtel Money | 105,855,000 | 106,723,000 | 119,439,000 |
| Azam Pesa | 1,686,684 | 1,775,008 | 2,301,520 |
| HaloPesa | 50,434,801 | 49,829,204 | 57,649,438 |
| T- Pesa | 185,584 | 127,583 | 152,044 |
| M-pesa | 225,346,758 | 219,317,001 | 252,285,075 |
| Mixx by Yas | 218,337,425 | 209,384,568 | 232,887,687 |
| **Jumla** | 601,846,252 | 587,156,364 | 664,714,764 |

### Jedwali 1.10.2b: Idadi ya usajili na miamala ya pesa mtandao kwa robo mwaka

| Robo mwaka | Idadi ya akaunti | idadi ya miamala |
|---|---|---|
| Machi 2025 | 66,542,276 | 1,366,334,366 |
| Juni 2025 | 68,059,290 | 1,392,683,175 |
| Septemba 2025 | 72,497,350 | 1,694,032,906 |
| Desemba 2025 | 76,466,691 | 1,853,717,380 |

### Jedwali 1.10.2c: Idadi ya usajili na miamala ya pesa mtandao kwa miaka mitano iliyopita

| Mwaka | Idadi ya akaunti | Idadi ya miamala |
|---|---|---|
| 2021 | 35,285,767 | 3,752,084,894 |
| 2022 | 40,953,496 | 4,195,899,414 |
| 2023 | 52,875,129 | 5,273,086,154 |
| 2024 | 63,207,569 | 3,737,202,434 |
| 2025 | 76,466,691 | 6,306,767,827 |

## 1.11 Ubora wa huduma za simu na intaneti

Vipimo vya ubora wa huduma (Quality of Service - QoS) ya simu na Intaneti zinazotolewa na mitandao ya simu nchini vilifanyika kuanzia Oktoba hadi Desemba 2025 kwa kuzingatia vigezo vya ubora wa huduma (QoS) na mbinu za vipimo zilizoainishwa kwenye Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Ubora wa Huduma), 2025.


Vipimo hivyo hufanyika kwenye huduma za sauti, data na jumbe fupi kutoka kwa watumiaji wa mwisho wanaotumia vifaa vya mawasiliano vinavyoweza kuunganishwa kwenye technolojia zote zinazopatikana (2G, 3G, 4G na 5G).

### 1.11.1 Upatikanaji wa mtandao

Upatikanaji wa mtandao ni kiashiria kinachoonesha upatikanaji wa mtandao wa simu wakati watumiaji wanataka kutumia huduma za mtandao huo. Lengo ni kufikia zaidi ya 99%.

Watoa huduma wote walifikia lengo kwenye maeneo yote ishirini ambapo vipimo vilifanyika kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.1.

**Chati 1.11.1: Upatikanaji wa Mtandao (%) (Lengo ni zaidi ya 99%)**





### 1.11.2 Simu zilizofanikiwa kuunganishwa

Simu zilizofanikiwa kuunganishwa hupimwa kwa asilimia ya simu ambazo ziliweza kuunganishwa baada ya kupiga. Lengo ni juu ya 98%.

Yas, Halotel na Vodacom zilifikia lengo kwenye maeneo kumi na saba kati ya maeneo kumi na nane ambapo vipimo vilifanyika. Airtel ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na sita kati ya maeneo kumi na saba, TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo sita kati ya maeneo kumi na saba yaliyopimwa kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.2.

**Chati 1.11.2: Simu zilizofanikiwa kuunganishwa**





## 1.11.3 Simu zilizokatika

Kipimo cha kiashiria hiki ni asilimia ya simu zinazokatika kwa sababu za kiufundi kabla ya wahusika kumaliza mazungumzo yao. Lengo ni chini ya 2%.

Vodacom na Yas zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na nane ambapo vipimo vilifanyika, Airtel na TTCL zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na saba na Halotel ilifikia lengo katika maeneo kumi na sita kati ya maeneo kumi na nane ambapo vipimo vilifanyika kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.3.

**Chati 1.11.3: Matokeo ya Simu zilizokatika**





## 1.11.4 Upatikanaji wa huduma ya 2G

Upatikanaji wa huduma ya 2G huonesha jinsi maeneo yaliyofikiwa na huduma hiyo na watoa huduma wa mtandao wa simu. Wateja hawawezi kupata huduma za mtandao wa simu za 2G katika maeneo ambayo hayana mtandao au yenye mtandao duni. Lengo la juu kwa teknolojia ya 2G ni -85 dBm.

Halotel ilifikia lengo katika maeneo yote kumi na nane ambapo vipimo vilifanyika, Vodacom na Airtel zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na saba na Yas ilifikia lengo katika maeneo yote tisa ambapo vipimo vilifanyika. TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo saba kati ya maeneo nane ambapo vipimo vilifanyika

kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.4.

**Chati 1.11.4: Matokeo linganishi kwenye upatikanaji wa huduma**





## 1.11.5 Upatikanaji wa huduma ya 3G

Upatikanaji wa huduma ya 3G huonesha jinsi maeneo yaliyofikiwa na huduma hiyo na watoa huduma wa mtandao wa simu. Wateja hawawezi kupata huduma za mtandao wa simu za 3G katika maeneo ambayo hayana mtandao au yenye mtandao duni. Lengo la juu kwa teknolojia ya 3G ni -95 dBm.

Vodacom, Yas na Halotel zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na nane ambapo vipimo vilifanyika, na Airtel na TTCL zilifikia lengo katika maeneo yete kumi na saba kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.5.

**Chati 1.11.5: Matokeo ya kulinganisha upatikanaji wa huduma ya 3G**





## 1.11.6 Upatikanaji wa huduma ya 4G

Upatikanaji wa huduma ya 4G huonesha jinsi maeneo yaliyofikiwa na huduma hiyo na watoa huduma wa mtandao wa simu. Lengo la juu kwa teknolojia ya 4G ni -100 dBm.

Watoa huduma wote walifikia lengo katika maeneo yote kumi na nane ambapo vipimo vilifanyika kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.6.

**Chart 1.11.6: Matokeo linganishi kwenye upatikanaji wa huduma ya 4G**





## 1.11.7 Kasi ya data

Kasi ya kupakua data ni kipimo cha kasi ya uhamishaji data kwenye mtandao. Hupima jinsi data inavyohamishwa haraka kutoka kwa itifaki (protocol) ya uhamishaji faili (File Transfer Protocol - FTP) hadi kwa kifaa cha mawasiliano ya simu. Lengo ni wastani kuwa sawa au zaidi ya 10,000 Kbps.

Yas, Airtel na Vodacom zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na nane ambapo vipimo vilifanyika. Halotel na TTCL zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na sita yaliyopimwa kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.7.

**Chati 1.11.7: Matokeo linganishi kwenye kasi ya data**





## 1.11.8 Muda wa kupata huduma ya data

Muda wa kupata huduma ya data hupimwa kwa muda ambao kifaa cha mtumiaji huchukua kutuma ombi na kupokea jibu kutoka kwenye seva. Lengo ni wastani kuwa chini ya 200ms.

Yas, Airtel na Vodacom zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na nane ambapo vipimo vilifanyika. Halotel na TTCL zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na sita yaliyopimwa kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.8.

**Chati 1.11.8: Matokeo linganishi ya muda wa kupata huduma ya data**





## 1.11.9 Muda wa kufika ujumbe mfupi wa maneno (SMS)

Muda wa kufika ujumbe mfupi wa maneno (SMS) inapima muda unaotumika kutoka ujumbe mfupi wa maneno (SMS) inavyotumwa mpaka inapofika kwenye simu husika. Lengo ni chini ya sekunde 2.

Yas, Halotel na Vodacom zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na nane ambapo vipimo vilifanyika. Aitel na TTCL zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na saba yaliyopimwa kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.9.

**Chati 1.11.9: Matokeo ya muda wa kufika ujumbe mfupi wa maneno**





## 1.11.10 Muda wa kuanzisha simu

Muda wa kuanzisha simu hupimwa kwa muda ambao simu inachukua kuunganishwa baada ya kupiga. Lengo ni chini ya sekunde 8.

Yas, Halotel na Vodacom zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na nane ambapo vipimo vilifanyika. Airtel na TTCL zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na saba yaliyopimwa kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.10.

**Chart 1.11.10: Matokeo ya kulinganisha muda wa kuanzisha simu**





## 1.11.11 Ubora wa sauti

Ubora wa Sauti ni kipimo cha utambuzi wa ubora wa sauti wakati wa mazungumzo ya simu. Kiwango cha alama ya ubora wa sauti ni kati ya 1 hadi 5, huku 1 ikiwa duni na 5 ikiwa ni ubora mzuri wa sauti. Lengo ni wastani wa sampuli zote za vipimo vya ubora wa sauti kuwa zaidi ya 4.

Vodacom na Halotel zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi ambapo vipimo vilifanyika. Airtel na TTCL zilifikisha lengo kwenye maeneo yote tisa, Yas ilifikisha lengo kwenye maeneo kumi tisa kati ya maeneo kumi ambapo vipimo vilifanyika kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.11.

**Chati 1.11.11: Matokeo ya muda wa kufika ujumbe mfupi wa maneno**




Matokeo ya upimaji wa ubora wa huduma za simu na Intaneti kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2025 yanaonesha kuwa Vodacom ilikuwa na 99.5%, Airtel 99.5%, Halotel 97.9%, TTCL 91.3%, na Yas 98.9%, kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali 1.11.

### Jedwali 1.11: Matokeo ya ubora wa huduma za simu na Intaneti kwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2025

| Mtoa huduma | Kiwango cha ufanisi |
|---|---|
| Vodacom | 99.5% |
| Airtel | 99.5% |
| Halotel | 97.9% |
| TTCL | 91.3% |
| Yas | 98.9% |
| **Wastani wa Sekta** | **97.4%** |

## 1.12 Majaribio ya ulaghai

Jedwali 1.12a linaonesha idadi ya majaribio ya ulaghai kwa kila mkoa katika robo mwaka iliyoishia Desemba 2025.

**Jedwali 1.12a: Majaribio ya ulaghai kwa mkoa**

| Mkoa | Airtel | Halotel | Yas | TTCL | Vodacom | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Tanzania Bara** | | | | | | |
| Rukwa | 135 | 589 | 199 | 1,950 | 571 | 3,444 |
| Morogoro | 387 | 127 | 1,118 | 5 | 1,468 | 3,105 |
| Dar es Salaam | 344 | 73 | 124 | 13 | 86 | 640 |
| Mbeya | 25 | 68 | 228 | 73 | 39 | 433 |
| Songwe | 5 | 52 | 60 | 16 | 98 | 231 |
| Arusha | 42 | 8 | 33 | 5 | 126 | 214 |
| Katavi | 4 | 74 | 23 | 72 | 1 | 174 |
| Kilimanjaro | 8 | 2 | 38 | 1 | 112 | 161 |
| Mwanza | 31 | 12 | 45 | 5 | 26 | 119 |
| Pwani | 21 | 33 | 42 | 1 | 4 | 101 |
| Tabora | 20 | 9 | 22 | 10 | 24 | 85 |
| Dodoma | 22 | 21 | 23 | 3 | 2 | 71 |
| Tanga | 20 | 8 | 36 | 3 | 3 | 70 |
| Manyara | 15 | 7 | 8 | 7 | 29 | 66 |
| Mara | 5 | 3 | 26 | 3 | 19 | 56 |
| Kagera | 7 | 2 | 31 | 2 | 10 | 52 |
| Ruvuma | 9 | 6 | 27 | 9 | 1 | 52 |
| Iringa | 9 | 12 | 18 | 6 | 5 | 50 |
| Shinyanga | 17 | 5 | 15 | 3 | 6 | 46 |
| Singida | 5 | 8 | 20 | 7 | 4 | 44 |
| Geita | 16 | 2 | 18 | 2 | 4 | 42 |
| Kigoma | 8 | 7 | 14 | 3 | 4 | 36 |
| Njombe | 1 | 8 | 12 | 10 | 2 | 33 |
| Mtwara | 6 | 2 | 19 | 4 | 0 | 31 |
| Simiyu | 5 | 4 | 9 | 7 | 1 | 26 |
| Lindi | 3 | 6 | 11 | 2 | 0 | 22 |
| **Zanzibar** | | | | | | |
| Mjini Magharibi | 4 | 1 | 24 | 0 | 0 | 29 |
| Kusini Pemba | 0 | 0 | 3 | 3 | 0 | 6 |
| Kaskazini Pemba | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 2 |
| Kusini Unguja | 0 | 0 | 5 | 0 | 0 | 5 |
| Kaskazini Unguja | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 4 |
| **Jumla** | **1,174** | **1,149** | **2,257** | **2,225** | **2,645** | **9,450** |


Kielelezo hapo chini kinaonesha majaribio ya ulaghai kwa kila mtoa huduma kwa robo ya mwaka inayoishia Septemba 2025 na Desemba 2025. Vodacom ilikuwa na idadi ya majaribio mengi zaidi ikilinganishwa na watoa huduma wengine, aidha Halotel ilikua na majaribio machache ikilinganishwa na watoa huduma

**Jedwali 1.12b: Majaribio ya ulaghai kwa kila mtoa huduma**

| Robo ya mwaka inayoishia | Airtel | Halotel | Yas | TTCL | Vodacom | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Desemba 2025 | 1,174 | 1,149 | 2,257 | 2,225 | 2,659 | 9,468 |
| Septemba 2025 | 1,559 | 2,272 | 2,454 | 2,219 | 3,971 | 12,475 |
| Badiliko | -25% | -49% | -8% | 0.3% | -33% | -24% |

Takwimu zinaonesha kuwa majaribio ya ulaghai kwa ujumla yamepungua kwa wastani wa 24%. Chati 1.12a inaonesha majaribio ya ulaghai kimkoa. Mikoa ya Rukwa na Morogoro ndiyo inayoongoza kwa majaribio ya ulaghai nchini.


**Chati 1.12a: Idadi majaribio ya ulaghai kimkoa kwa robo mwaka inayoishia Desemba 2025**



## Jedwali 1.12c: Majaribio ya ulaghai kiwilaya kwa mikoa minne inayoongoza

| Mkoa | Wilaya | Majaribio ya ulaghai |
|---|---|---|
| Rukwa | Sumbawanga | 1,694 |
| | Nkasi | 894 |
| | Kalambo | 856 |
| Morogoro | Morogoro | 46 |
| | Mvomero | 16 |
| | Gairo | 6 |
| | Kilosa | 57 |
| | Kilombero | 2,740 |
| | Ulanga | 143 |
| | Malinyi | 97 |
| Dar es Salaam | Ilala | 143 |
| | Kinondoni | 199 |
| | Temeke | 106 |
| | Ubungo | 173 |
| | Kigamboni | 19 |
| Mbeya | Mbeya | 229 |
| | Chunya | 27 |
| | Mbarali | 64 |
| | Rungwe | 100 |
| | Kyela | 13 |

## Chati 1.12b: Mgawanyo wa asilimia ya majaribio ya ulaghai mtandaoni kwa kila mtoa huduma



## 1.13 Leseni za huduma ya Mawasiliano ya simu na intaneti

| Mawasiliano ya simu na Intaneti | | |
|---|---|---|
| **Aina ya leseni** | **Idadi ya leseni** | |
| | **Septemba 2025** | **Desemba 2025** |
| Network Facilities Licences | 47 | 48 |
| Network Services Licences | 23 | 24 |
| Application Services Licences | 147 | 159 |
| Aircraft Stations | 194 | 194 |
| Amateur Stations | 16 | 17 |
| Fixed VSAT Terminals | 26 | 21 |
| Mobile VSAT Terminals | 1 | - |
| Satellite Ground Earth Stations | - | - |
| Ship Stations | 32 | 42 |
| HF Radio Stations | 16 | 16 |
| VHF- UHF Radio Repeaters | - | - |
| VHF - UHF Radio Station with Pair of Frequency | 122 | 125 |
| VHF - UHF Radio Station with Single Frequency | 181 | 184 |
| Numbering | 530 | 515 |

## 1.14 Vyeti

| Aina ya cheti na idadi | | |
|---|---|---|
| **Aina ya cheti** | **Idadi ya vyeti** | |
| | **Septemba 2025** | **Desemba 2025** |
| Global Maritime Distress and Safety Systems | 288 | 316 |
| Type Approval | 5,412 | 5,538 |
| Registration for Satellite Mobile Phones | 51 | 51 |

# Sura ya pili

## Huduma za Utangazaji



# 2. Huduma za Utangazaji


Sehemu hii inawasilisha takwimu za huduma za televisheni kwa njia ya mitambo iliyosimikwa ardhini (DTT), setelaiti (DTH), na kwa njia ya waya (Cable TV), pamoja na maeneo ya kijografia na idadi ya watu waliofikiwa na mawimbi ya huduma za utangazaji. Pia inatoa tathmini ya uzingatiaji wa ubora wa huduma.

## 2.1 Visimbuzi vilivyolipiwa angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu

Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita ili kupata huduma za utangazaji za televisheni imepungua kwa asilimia 8.5 kama invyooneshwa kwenye kielelezo hapo chini.

| Kufikia Septemba 2025 | Kufikia Desemba 2025 | |
|---|---|---|
| **Milioni 2.3** | **Milioni 2.1** | **8.5%** ↓ |

**Kielelezo 2.0: Mgawanyiko wa visimbuzi vilivyolipiwa**




Kwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2025, Azam Media Limited ilikua na idadi kubwa ya visimbuzi ikifuatiwa na Star Media Limited kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali 2.1.


**Jedwali 2.1: Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa kwa kila mtoa huduma kufikia Desemba 2025**

| Mtoa huduma | Visimbuzi vya DTT | Visimbuzi vya DTH | Jumla ya visimbuzi vilivyolipiwa |
|---|---|---|---|
| Azam Media Limited | 317,332 | 1,112,525 | 1,429,857 |
| Basic Transmissions Limited (Continental) | 33,763 | 27,974 | 61,737 |
| Multichoice Tanzania Limited (DStv) | N/A | 212,663 | 212,663 |
| Star Media Limited | 188,661 | 210,360 | 399,021 |
| Zuku | N/A | 16,277 | 16,277 |
| **Jumla** | **539,756** | **1,579,799** | **2,119,555** |

Agape Associates Limited na Basic Transmissions Limited (Digitek) hawakuwa na visimbuzi vilivyolipiwa angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu.

Ramani 2.1 inaonesha idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa vifurushi kwa kila mkoa. Dar es Salaam ina visimbuzi vingi (682,767), ikifuatiwa na Mwanza (175,738), Mbeya (138,403), Arusha (129,913) na mikoa mingine ni kama ilivyo oneshwa kwenye ramani.


**Ramani 2.1: Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa vifurushi kwa kila mkoa**




## 2.2 Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya

Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya (Cable TV subscriptions) zimeongezeka kwa 2% kutoka 16,957 kwa robo mwaka inayoishia Septemba 2025 na kufikia 17,280 kwa robo mwaka inayoishia Desemba 2025.

**Kielelezo 2. 2: Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya**



| Kufikia Septemba 2025 | Kufikia Desemba 2025 |
|---|---|
| 16,957 | 17,280 |

2%

Idadi ya televisheni kwa kila mkoa katika kipindi husika imeoneshwa kwenye Chati 2.2.

**Chati 2.2: Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya kufikia Desemba 2025**




Kwa mikoa yote Tanzania Bara, Shinyanga inaongoza kwa kuwa na televisheni nyingi zinazopokea maudhui kwa njia ya waya (4,115), ikifuatiwa na Tabora (2,015), Mwanza (1,875), na Dar es Salaam (1,655). Mikoa yenye televisheni chache kwa njia ya waya ni Katavi (49), Rukwa (76) na Ruvuma (95).

Mwenendo wa idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya zimeoneshwa kwenye Jedwali 2.2a na 2.2b.

**Jedwali 2.2a: Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya kwa robo mwaka**

| | Machi 2025 | Juni 2025 | Septemba 2025 | Desemba 2025 |
|---|---|---|---|---|
| Usajili | 17,185 | 17,657 | 16,957 | 17,280 |

**Jedwali 2.2b: Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita**

| | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Usajili | 19,739 | 22,295 | 16,223 | 16,767 | 17,280 |

## 2.3 Ueneaji wa huduma za utangazaji

Takwimu zinaonesha kuna utofauti wa ueneaji wa huduma za utangazaji kwa njia ya DTT, DTH na redio kama inavyoonekana kwenye Jedwali 2.3.

**Jedwali 2.3: Ueneaji wa huduma za utangazaji hadi kufikia Desemba 2025**

| Kiashiria | Septemba 2025 | Desemba 2025 |
|---|---|---|
| % ya watu waliofikiwa na mawimbi na DTT | 58.00% | 58.00% |
| % ya watu waliofikiwa mawimbi na DTH | 100.00% | 100.00% |
| % ya watu waliofikiwa na mawimbi ya redio za FM | 83.92% | 83.94% |
| % ya eneo lililofikiwa mawimbi na DTT | 33.00% | 33.00% |
| % ya eneo lililofikiwa mawimbi na DTH | 100.00% | 100.00% |
| % ya eneo lililofikiwa na mawimbi redio za FM | 59.13% | 59.15% |

## 2.4 Utekelezaji wa masharti ya leseni za utangazaji

Ufuatiliaji wa maudhui kwa watoa huduma za utangazaji wa kitaifa nchini (Televisheni na Redio) ulifanyika kuanzia Oktoba hadi Desemba 2025 kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Ubora wa Huduma), 2025.

Watoa huduma za utangazaji wa kitaifa wanatakiwa kutoa ratiba ya vipindi (muda, mpango, na idadi) na kuzingatia ratiba ya vipindi waliyoitoa.

### 2.4.1 Uwasilishaji na uzingatiaji wa ratiba ya vipindi

Uzingatiaji wa uwasilishaji wa mpangilio wa vipindi na kufuata ratiba kwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2025 umeonyeshwa kwenye Jedwali 2.4.1a na 2.4.1b.

**Jedwali 2.4.1a: Uwasilishaji na uzingatiaji wa mpango wa vipindi vya televisheni kwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2025**

| TV | Uwasilishaji wa ratiba ya vipindi | Uzingatiaji wa ratiba ya vipindi |
|---|---|---|
| ITV | Imekidhi | Haijakidhi |
| UTV | Haijakidhi | Haijakidhi |
| Tumaini TV | Haijakidhi | Haijakidhi |
| Channel Ten Television | Imekidhi | Haijakidhi |
| East Africa TV | Imekidhi | Imekidhi |
| Star TV Tanzania | Imekidhi | Imekidhi |
| TBC 1 | Imekidhi | Imekidhi |
| TV Imaan | Imekidhi | Haijakidhi |
| Arise and Shine TV | Imekidhi | Haijakidhi |
| WRM TV | Imekidhi | Haijakidhi |
| Clouds TV | Imekidhi | Haijakidhi |
| Hope Channel Tanzania | Haijakidhi | Haijakidhi |
| Upendo TV | Imekidhi | Haijakidhi |
| Mahaasin TV | Imekidhi | Imekidhi |
| Channel Ten Plus | Imekidhi | Haijakidhi |
| TVE | Haijakidhi | Haijakidhi |

**Jedwali 2.4.1b: Uwasilishaji na uzingatiaji wa mpango wa vipindi vya redio kwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2025**

| Redio | Uwasilishaji wa ratiba ya vipindi | Uzingatiaji wa ratiba ya vipindi |
|---|---|---|
| Radio One | Imekidhi | Imekidhi |
| TBC Taifa | Imekidhi | Imekidhi |
| Adventist World Radio (AWR) | Imekidhi | Imekidhi |
| Clouds FM | Haijakidhi | Haijakidhi |
| East Africa Radio | Imekidhi | Imekidhi |
| EFM | Imekidhi | Haijakidhi |
| Wasafi FM | Haijakidhi | Haijakidhi |
| Magic FM | Imekidhi | Imekidhi |
| TBC International | Imekidhi | Imekidhi |
| Radio Free Africa | Imekidhi | Imekidhi |
| Bongo FM | Imekidhi | Haijakidhi |
| Radio Maria | Imekidhi | Imekidhi |

## 2.4.2 Uanuai wa vipindi, maudhui ya elimu na uzingatiaji wa uwasilishaji wa habari

Uzingatiaji wa uanuai wa vipindi, utoaji wa maudhui ya elimu na viwango vya uwasilishaji wa habari kwa vipindi vya televisheni na redio kwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2025 umeoneshwa kwenye Jedwali 2.4.2a na 2.4.2b, mtawalia.

Watoa huduma za utangazaji wenye leseni za kitaifa (national broadcasters) wanatakiwa kutoa maudhui anuai, elimu na burudani ili kukidhi mahitaji ya rika tofauti na tamaduni.

**Jedwali 2.4.2a: Uanuai wa vipindi vya televisheni kwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2025**

| TV | Utofauti wa vipindi | Maudhui ya elimu | Uzingatiaji wa dakika tisini wa habari |
|---|---|---|---|
| ITV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| UTV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Tumaini TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Channel Ten Television | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| East Africa TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Star TV Tanzania | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| TBC 1 | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| TV Imaan | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Arise and Shine TV | Imekidhi | Imekidhi | Haijakidhi |
| WRM TV | Imekidhi | Haijakidhi | Haijakidhi |
| Clouds TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Hope Channel Tanzania | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Upendo TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Mahaasin TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Channel Ten Plus | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| TVE | Haijakidhi | Haijakidhi | Imekidhi |

**Jedwali 2.4.2b: Uanuai wa vipindi vya redio kwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2025**

| Redio | Utofauti wa vipindi | Maudhui ya elimu | Uzingatiaji wa dakika tisini wa habari |
|---|---|---|---|
| Radio One | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| TBC Taifa | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Adventist World Radio (AWR) | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Clouds FM | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| East Africa Radio | Imekidhi | Imekidhi | Haijakidhi |
| EFM | Imekidhi | Imekidhi | Haijakidhi |
| Wasafi FM | Imekidhi | Imekidhi | Haijakidhi |
| Magic FM | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| TBC International | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Radio Free Africa | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Bongo FM | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Radio Maria | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |

### 2.4.3 Uzingatiaji wa maudhui ya ndani (local content)

Watoa huduma za utangazaji wenye leseni za kitaifa (national broadcasters) wanatakiwa kuhakikisha kwamba asilimia 60 ya vipindi vyao vimetengenezwa ndani ya nchi, ili kuchagiza utamaduni, lugha, na maudhui ya ndani ya nchi. Matokeo ya upimaji ya uzingatiaji wa maudhui ya ndani kwenye vipindi vya televisheni na redio kwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2025 yameoneshwa kwenye Jedwali 2.4.3a na Jedwali 2.4.3b.

**Jedwali 2.4.3a: Uzingatiaji wa maudhui ya ndani kwenye vipindi vya televisheni kwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2025**

| TV | Yenye manufaa kwa jamii | Lugha (Kiswahili au Kiingereza) | 60% ya uzalishaji wa maudhui ya ndani |
|---|---|---|---|
| ITV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| UTV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Tumaini TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Channel Ten Television | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| East Africa TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Star TV Tanzania | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| TBC 1 | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| TV Imaan | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Arise and Shine TV | Imekidhi | Haijakidhi | Imekidhi |
| WRM TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Clouds TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Hope Channel Tanzania | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Upendo TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Mahaasin TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Channel Ten Plus | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| TVE | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |

**Jedwali 2.4.3b: Uzingatiaji wa maudhui ya ndani kwenye vipindi vya redio kwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2025**

| Redio | Yenye manufaa kwa jamii | Lugha (Kiswahili au Kiingereza) | 60% ya uzalishaji wa maudhui ya ndani |
|---|---|---|---|
| Radio One | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| TBC Taifa | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Adventist World Radio (AWR) | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Clouds FM | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| East Africa Radio | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| EFM | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Wasafi FM | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Magic FM | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| TBC International | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Radio Free Africa | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Bongo FM | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Radio Maria | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imechukua na itaendelea kuchukua hatua stahiki za kiudhibiti kwa watoa huduma wote walioshindwa kukidhi vigezo vilivyoainishwa kwa mujibu wa kanuni husika.

## 2.5 Leseni za huduma za Utangazaji

| Aina ya leseni | Idadi ya leseni | |
|---|---|---|
| | **Septemba 2025** | **Desemba 2025** |
| National Content Television (FTA) Licences | 20 | 21 |
| District Content Television (FTA) Licences | 21 | 21 |
| National Content Radio Licences | 14 | 14 |
| Regional Content Radio Licences | 37 | 37 |
| District Content Radio Licences | 185 | 188 |
| Community Radios | 19 | 19 |
| National Content Televisions by Subscription | 30 | 30 |
| District Content Televisions by Subscription | 1 | 1 |
| National Content ( support services) | 3 | 3 |
| Online Content Aggregators | 6 | 6 |
| Weblogs (Blogs) | 72 | 77 |
| Online Radios | 13 | 13 |
| Online Televisions | 216 | 222 |
| Cable Televisions | 51 | 55 |

# Sura ya tatu

## Huduma za Posta na Usafirishaji wa vifurushi na vipeto



# 3. Huduma za Posta na Usafirishaji wa Vifurushi na Vipeto

Sehemu hii inawasilisha takwimu za masanduku ya posta, wateja, huduma ya posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto, zilizotumwa na kupokelewa, kwenda na kutoka ndani ya nchi, Afrika Mashariki (EA) na mataifa mengine (RoW).

## 3.1 Idadi ya masanduku ya posta

Shirika la Posta Tanzania (TPC) linatoa huduma za msingi za posta za masanduku na mifuko binafsi ya barua kwa watu binafsi na kampuni. Idadi ya masanduku na mifuko binafsi katika kipindi cha mwezi Oktoba hadi Desemba 2025, ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 3.1.

**Jedwali 3.1: Masanduku na mifuko binafsi ya barua**

| Mwezi | Masanduku ya barua | Mifuko binafsi ya barua | Jumla |
|---|---|---|---|
| Oktoba | 158,006 | 67 | **158,073** |
| Novemba | 158,006 | 67 | **158,073** |
| Desemba | 158,006 | 67 | **158,073** |

## 3.2 Wateja wa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto

Idadi ya wateja wa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto katika kipindi cha mwezi Septemba hadi Desemba 2025 imeoneshwa kwenye Jedwali 3.2.

**Jedwali 3.2: Idadi ya wateja wa huduma ya usafirishaji wa vifurushi/vipeto**

| Mwezi | Kampuni/Taasisi | Wateja binafsi | Jumla |
|---|---|---|---|
| Oktoba | 608 | 64,178 | **64,786** |
| Novemba | 682 | 61,860 | **62,542** |
| Desemba | 729 | 71,762 | **72,491** |

Jedwali 3.2 inaonesha kuwa wateja binafsi ni wengi zaidi kuliko wateja wa makampuni/taasisi.

## 3.3 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa

### 3.3.1 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa ndani ya nchi


Takwimu zinaonesha barua zilitumwa zaidi katika kipindi cha robo mwaka kilichoishia Desemba 2025, ikifuatiwa na vifurushi. Mizigo (Cargo) imetumwa kwa idadi ndogo zaidi katika kipindi hicho. Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa katika kipindi husika zimeoneshwa kwenye Jedwali 3.3.1.

### Jedwali 3.3.1: Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa ndani ya nchi kwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2025

| Mwezi | Barua | Vifurushi | Vipeto | Nyaraka | Mizigo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Oktoba | 47,968 | 48,903 | 14,575 | 38,295 | 736 | 150,477 |
| Novemba | 66,255 | 49,018 | 11,418 | 34,683 | 3,104 | 164,478 |
| Desemba | 111,504 | 61,168 | 10,895 | 55,025 | 714 | 239,306 |
| Jumla | 225,727 | 159,089 | 36,888 | 128,003 | 4,554 | 554,261 |

Mgawanyo wa idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa na TPC na watoa huduma wengine wa huduma za usafirishaji ndani ya nchi ilikua ni (61%) 337,434 kwa TPC na (39%) 216,827 kwa watoa huduma binafsi kama ilivyooneshwa katika Chati 3.3.1.

### Chati 3.3.1: Mgawanyo wa idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa ndani ya nchi




## 3.3.2 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi

Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi kupitia TPC na watoa huduma wengine wa huduma ya usafirishaji katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2025 imeoneshwa kwenye jedwali 3.3.2a.

### Jedwali 3.3.2a: Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi kwa mtoa huduma

| Watoa huduma | Jul - Sept 2025 | Okt - Des 2025 |
|---|---|---|
| TPC | 24,649 | 27,877 |
| Watoa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto | 2,830 | 2,188 |
| Jumla | 27,479 | 30,065 |

Jedwali 3.3.2b linaonesha idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi. Takwimu zinaonesha kuwa barua zimetumwa zaidi nje ya nchi katika robo mwaka iliyoishia Desemba 2025, ikifuatiwa na nyaraka.

### Jedwali 3.3.2b: Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi

| Mwezi | Barua | Vifurushi | Vipeto | Nyaraka | Mizigo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Oktoba | 8,292 | 172 | 92 | 300 | 2 | 8,858 |
| Novemba | 8,079 | 250 | 116 | 861 | 0 | 9,306 |
| Desemba | 10,367 | 343 | 146 | 1,036 | 9 | 11,901 |
| Jumla | 26,738 | 765 | 354 | 2,197 | 11 | 30,065 |

## 3.4 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa

### 3.4.1 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka ndani ya nchi

Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kupitia TPC na watoa huduma wengine wa usafirishaji wa vifurushi na vipeto imeoneshwa kwenye jedwali 3.4.1.

**Jedwali 3.4.1: Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa ndani ya nchi kwa robo ya mwaka iliyoishia Desemba 2025**

| Mwezi | Barua | Vifurushi | Vipeto | Nyaraka | Mizigo | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Oktoba | 212,301 | 67,414 | 13,576 | 18,771 | 670 | 312,732 |
| Novemba | 153,419 | 42,594 | 10,424 | 36,036 | 2,976 | 245,449 |
| Desemba | 160,906 | 48,362 | 9,562 | 36,805 | 246 | 255,881 |
| Jumla | 526,626 | 158,370 | 33,562 | 91,612 | 3,892 | 814,062 |

### 3.4.2 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi

Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha mwezi Oktoba hadi Desemba 2025 imeoneshwa kwenye jedwali 3.4.2a.

**Jedwali 3.4.2a: Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi katika robo mwaka iliyoishia Desemba 2025**

| Watoa huduma | Jul - Sept 2025 | Okt - Des 2025 |
|---|---|---|
| TPC | 55,605 | 44,069 |
| Watoa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto | 10,086 | 2,293 |
| Jumla | 65,691 | 46,362 |


Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi zimeoneshwa kwenye Jedwali 3.4.2b. Barua kutoka nje ya nchi zimepokelewa kwa idadi kubwa zaidi ikilinganisha na bidhaa nyingine katika robo ya mwaka iliyoishia Desemba 2025, wakati mizigo kutoka nje ya nchi ilipokelewa kwa idadi ndogo zaidi katika kipindi husika.

**Jedwali 3.4.2b: Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi katika robo mwaka iliyoishia Desemba 2025**

| Mwezi | Barua | Vifurushi | Vipeto | Nyaraka | Mizigo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Oktoba | 10,747 | 860 | 3,699 | 412 | 7 | 15,725 |
| Novemba | 9,725 | 843 | 3,979 | 376 | 30 | 14,953 |
| Desemba | 9,228 | 988 | 4,419 | 1,039 | 10 | 15,684 |
| Jumla | 29,700 | 2,691 | 12,097 | 1,827 | 47 | 46,362 |

Mgawanyo wa idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa na kupokelewa unaonesha kuwa Tanzania ilituma bidhaa za kiposta chache zaidi nje ya nchi (29%) kuliko ilivyopokea (71%) kama ilivyooneshwa kwenye Chati 3.4.

**Chati 3.4: Mgawanyo wa bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi na kupokelewa kutoka nje ya nchi**




## 3.5 Ubora wa huduma za Posta na Usafirishaji wa vifurushi na vipeto

Katika kipindi cha robo mwaka kilichoishia Desemba 2025, vipimo vya Ubora wa Huduma (QoS) vilifanyika katika kanda A, B na C ili kutathmini namna huduma za usafirishaji wa vifurushi na vipeto zilivyokidhi viwango vya utoaji huduma vilivyowekwa kwenye kanuni za ubora.

Kanda A (Inter-Town Zone A) inayojumuisha miji ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Dodoma, Iringa, Zanzibar na Mwanza kiwango kinahitaji 90% ya bidhaa zipokelewe siku inayofuata (D+1). Kanda B (Inter-Town Zone B), inayojumuisha miji ya Mbeya, Njombe, Ruvuma, Mtwara, Singida na Lindi, na Kanda C (Inter-Town Zone C) inayojumuisha miji ya Tabora na Geita ambapo kote kiwango kinahitaji 90% ya bidhaa zipokelewe ndani ya siku mbili (D+2). Matokeo ya upimaji yameoneshwa kwenye jedwali 3.5a na 3.5b.

**Jedwali 3.5a: Ubora wa huduma za usafirishaji wa vifurushi na vipeto kanda A (90% ya bidhaa zipokelewe siku inayofuata (D+1)**

| Mtoa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto ndani ya nchi | Kasi ya uwasilishaji kwa eneo la kanda A |
|---|---|
| Air Tanzania Company Limited | Imekidhi |
| Zan Fast Ferries Company Limited | Imekidhi |
| Precision Air Services Plc | Imekidhi |
| M/S Azam Marine Company Limited | Imekidhi |
| Anthony Bosco Madeira T/A Madeira Courier Services | Imekidhi |
| Sga Cash In Transit (T) Limited | Imekidhi |
| Urban Eagle | Imekidhi |
| Kapilla Group Limited | Imekidhi |
| Tutume Worldwide Limited | Imekidhi |
| HOZAC LOGISTICS COMPANY LTD | Imekidhi |
| Abc Upper Class & Transportation Limited | Imekidhi |
| Ndengaro Company Limited | Imekidhi |
| H&N Courier Express Limited | Haijakidhi |
| Marathon Logistics Limited | Haijakidhi |
| Jonz Express Logistics And Supplies Limited | Haijakidhi |
| Couriemate Tanzania Limited | Haijakidhi |

| Mtoa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto ndani ya nchi | Kasi ya uwasilishaji kwa eneo la kanda A |
|---|---|
| Kimua Company Limited | Haijakidhi |
| Kimbinyiko International Co. Ltd | Haijakidhi |
| Rangel Logistics Tanzania Limited | Haijakidhi |
| Dhl Tanzania Limited | Haijakidhi |

**Jedwali 3.5a: Ubora wa huduma za usafirishaji wa vifurushi na vipeto kanda B na C (90% ya bidhaa zipokelewe ndani ya siku mbili (D+2)**

| Mtoa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto ndani ya nchi | Kasi ya uwasilishaji kwa eneo la kanda B na C (D+2(90%)) |
|---|---|
| Air Tanzania Company Limited | Imekidhi |
| Precision Air Services Plc | Imekidhi |
| Malitabu Musa Ntamala T/A Skygo Express | Imekidhi |
| Sga Cash In Transit (T) Limited | Imekidhi |
| Kapilla Group Limited | Imekidhi |
| Abc Upper Class & Transportation Limited | Imekidhi |
| Marathon Logistics Limited | Imekidhi |
| Ndengaro Company Limited | Haijakidhi |
| Couriemate Tanzania Limited | Haijakidhi |
| Kimbinyiko International Co. Ltd | Haijakidhi |
| Jonz Express Logistics And Supplies Limited | Haijakidhi |
| HOZAC LOGISTICS COMPANY LTD | Haijakidhi |
| Rangel Logistics Tanzania Limited | Haijakidhi |
| H&N Courier Express Limited | Haijakidhi |
| Dhl Tanzania Limited | Haijakidhi |
| Kimua Company Limited | Haijakidhi |
| Gateway Global Freight Limited | Haijakidhi |

TCRA imechukua na itaendelea kuchukua hatua stahiki za kiudhibiti kwa watoa huduma wote walioshindwa kukidhi vigezo vilivyoainishwa kwa mujibu wa kanuni husika.

## 3.6 Leseni za huduma ya posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto

| Aina ya leseni | Idadi | |
|---|---|---|
| | Septemba 2025 | Desemba 2025 |
| International Courier | 6 | 6 |
| Intercity Transporters | 65 | 62 |
| Intracity Courier | 12 | 11 |
| Domestic Courier | 64 | 69 |
| Public Postal | 1 | 1 |

# 4. Hitimisho

Sekta ya mawasiliano imeendelea kuonesha ukuaji mkubwa katika robo ya mwaka iliyoishia Desemba 2025, ikionesha umuhimu wake katika kuendeleza mabadiliko ya kidijitali na maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini. Sekta imeendelea kuwa thabiti na bunifu, ikichochewa na ongezeko la uwekezaji, uvumbuzi, na matumizi ya huduma mbalimbali za mawasiliano, utangazaji, posta na usafirishaji wa vifurushi.

Katika huduma za mawasiliano ya simu na intaneti, kulikuwa na ongezeko endelevu la usajili, matumizi ya pesa mtandao, na matumizi ya data yanayotokana na kuenea kwa miundombinu ya mtandao wa intaneti ya kasi na kuongezeka kwa matumizi ya vifaa janja. kumekuwa na ongezeko endelevu la usajili wa laini za simu na matumizi ya data kwa asilimia 7.7 na asilimia 9.5, mtawalia. Aidha, matumizi ya huduma za sauti yamepungua kwa asilimia 0.3. Uendelezaji wa mitandao ya 4G (94.2%) na usambazaji wa mitandao ya 5G (30.1%) umeimarisha upatikanaji wa huduma za intaneti ya kasi na kuweka msingi imara wa ushiriki wa nchi katika uchumi wa kidijitali. Usajili wa intaneti uliongezeka kwa asilimia 3.2 na kufikia milioni 58.1. Huduma za pesa mtandao zimeendelea kukua ambapo idadi ya akaunti za pesa mtandao imeongezeka kwa asilimia 6.7 na hivyo kuimarisha ujumuishwaji wa huduma za kifedha.

Sekta ya utangazaji imekuwa na mchango mkubwa katika kusambaza taarifa, kukuza utamaduni, na kuimarisha umoja wa kitaifa. Idadi ya watu waliofikiwa na mawimbi ya DTT na FM imefikia asilimia 58 na 83.9, mtawalia, ambayo ni sawa na ilivyokuwa katika robo mwaka iliyoishia Septemba 2025. Kwa upande mwingine, idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa kifurushi (active decoders) imepungua kwa asilimia 8.5, na kufikia milioni 2.1 katika kipindi husika.

Huduma za posta na usafirishaji wa vifurushi zimeendelea kubadilika sambamba na ukuaji wa teknolojia na biashara mtandaoni. Sekta hii inaendelea kuwa kiungo muhimu katika kuwaunganisha wananchi na biashara, hasa katika maeneo ya vijijini, kupitia utoaji wa huduma za barua, vifurushi na usafirishaji wa mizigo kwa ufanisi.

Kwa ujumla, matokeo ya robo mwaka inayoishia Desemba 2025 yanaonesha kasi endelevu ya ukuaji wa sekta ya mawasiliano kuelekea Tanzania iliyounganishwa zaidi, jumuishi na yenye uchumi wa kidijitali. TCRA itaendelea kuweka mazingira wezeshi yanayochochea uwekezaji katika miundombinu, ubunifu, na ukuaji endelevu wa sekta ya mawasiliano kwa mujibu wa vipaumbele vya maendeleo vya Taifa na dira ya uchumi wa kidijitali.

Mawasiliano Towers,
20 Sam Nujoma Road,
14414 Dar es Salaam, Tanzania.
Email: dg@tcra.go.tz

@tcra_tanzania